ثَـــــنَاءُ خَـلِـــــيْفَةِ

عليِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ

عَلَى الْخَلِيْفَتَيْنِ أَبِي بَكْرٍ وَعُمَرَ - رَضِيَ اللّٰهُ عَنْهُمْ أَجْمَعِيْنَ -

KUWASIFU KWAKE

ALLY BIN ABI TWALIB

MAKHALIFA WAWILI ABUBAKAR NA OMAR (ALLAAH AWARIDHIE)

Tarjama

Abu Halima Arafat bin Mahmoud

Utangulizi wa Mtunzi

Kila sifa njema anastahiki Mola wa viumbe wote, na -swala na salamu zimshukie- Mtume wetu Muhamad, Aliye Mbora wa Mitume na Manabii wote, na pia ziwashukie Jamaa na Maswahaba wake wote.

Baada ya hayo: Hakika Maswahaba ni watu bora katika Umma huu baada ya Manabii, Allaah Ta'alaa amewakirimu kwa kusuhubiana na Mtume wake -swala na salamu zimshukie-, wakamuamini na kumfuata, wakamtia nguvu na kumnusuru, na wakamkomboa kwa kutoa fidia za mali na roho zao, na wakaibeba risala yake na kuifikisha (kila pande ya dunia).

Na hao Maswahaba ni kama alivyosema Abdullaahi Bin Masoud -Allaah amridhie-: **"Watakasifu zaidi wa umma huu kwa mioyo, watambuzi zaidi kwa kielimu, wachache zaidi kwa kujikalifisha, wenye kunyooka zaidi kwa mwuongozo, wazuri zaidi kwa hali, Allaah amewachagua ili kusuhubiana na Mtume wake -swala na salamu zimshukie-, basi tambueni fadhila zao na wafuateni katika athari zao, kwa sababu wao walikuwa katika mwuongozo ulionyooka"[1].**

Na katika misingi ya Ahlus Sunna Wal-Jamaa' ni kusalimika kwa mioyo yao na ndimi zao na kutowatusi Maswahaba wa Mtume -swala na salamu zimshukie- wala kuwachukia na kuwakashifu, na kuwatia dosari, kama Allaah alivyosema:

﴿ وَٱلَّذِينَ جَآءُو مِنۢ بَعۡدِهِمۡ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لَنَا وَلِإِخۡوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا بِٱلۡإِيمَٰنِ وَلَا تَجۡعَلۡ فِي قُلُوبِنَا غِلّٗا لِّلَّذِينَ ءَامَنُواْ رَبَّنَآ إِنَّكَ رَءُوفٞ رَّحِيمٌ ﴾

"Na wale ambao wamekuja baada yao wanasema: Ewe Mola wetu tusamehe sisi na ndugu zetu waliotangulia katika Imani wala usijaalie katika nyoyo zetu kinyongo kwa wale walio amini. Ewe Mola wetu hakika wewe ni Mpole Mwenye huruma"[2].

---

[1]- [Jaamiul Bayaanil ilmi] (Jz. 2, Uk. 947). [Al-Qurtubi] (Jz. 1, Uk. 60), [Al-Hilya] (Jz. 1, Uk. 305).

[2]- Surata Al-Hasri/10.

Hakika waliishi Maswahaba pamoja na Ahlul Bayt katika maisha yaliyo tawaliwa na kupendana, kuhurumiana na kuheshimiana, tafauti na madai ya Shia Ithnaasharia, ambao wametunga historia na kuweka hadithi za uwongo ambazo zinaleta dhana ya uwepo wa uadui baina ya Maswahaba na Ahlul Bayt (jamaa wa nyumba ya Mtume -swala na salamu zimshukie-.

Na kuna kundi kubwa la wanachuoni walio wabora wameandika vitabu vingi vinavyoelezea mahusiano baina ya Maswahaba na Ahlul Bayt na kwamba walikuwa na mafungano ya udugu, ukwe, na kusaidiana.

Isipokuwa mimi nakusudia katika risala yangu hii kuzungumzia mahusiano yaliyopo baina ya Abubakar, Omar na Ally -Allaah amridhie- kwa sababu ndio mahala unapozunguka uongo na uzushi wa mashia.

Kwa ajili hiyo nimetaka kubainisha juu ya mahusiano hayo kwa nukuu za kisheria, kadhalika ushahidi wa kiakili, na kubainisha mapenzi ya Ally juu ya Abubakar na Omar -Allaah awaridhie- na kuwasifia kwake, kiasi cha kubatilisha uwongo na uzushi wa (mashia) kuhusiana na historia ya Maswahaba wa Mtume -swala na salamu zimshukie- na sera yao tukufu.

Ninamuomba Allaah aitakase amali yangu hii kwa kutafuta wajhi wake ulio mkarmu, na ajaalie ni wenye kumnufaisha ndugu msomaji.

Swala na salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake pamoja na Maswahaba wote.

Amenadika:

Ali Bin Abdillaah Al-Ammaari

20/ramadhani/1439H.

KIPAMBANUZI CHA KWANZA

KUBAINISHA NAFASI YA MASWAHABA WOTE KWA UJUMLA NA (NAFASI YA) MAKHALIFA WATATU

ABUBAKAR, OMAR NA UTHMAN –Allaah amridhie–

NUKTA YA KWANZA
NAFASI YA MASWAHABA -Allaah amridhie-

Maswahaba ni watu wenye cheo na nafasi kubwa kwa waislamu, wao ndio kiunganisha ambacho kimetunukulia sisi Qur'an na Sunnah (Hadithi), na Allaah -'Azza Wajalla- amewasifu wao sehemu nyingi ndani ya kitabu chake kitakatifu (Qur'an). Amesema Allaah:

﴿ وَٱلسَّٰبِقُونَ ٱلۡأَوَّلُونَ مِنَ ٱلۡمُهَٰجِرِينَ وَٱلۡأَنصَارِ وَٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُم بِإِحۡسَٰنٖ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُ وَأَعَدَّ لَهُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي تَحۡتَهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدٗاۚ ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ ﴾

"Na wale waliotangulia, wa mwanzo, katika Muhajirina na Ansar, na waliowafuata wao kwa wema, Allaah ameridhika na wao wameridhika na Yeye, na amewaandalia wao bustani (ya pepo) ambayo inapita mito chini yake hali ya kukaa milele humo. Huko ndiko kufaulu kukubwa"[(3)]. Na Aya hii inawaenea Maswahaba wote.

Na Allaah anasema:

﴿ مُّحَمَّدٞ رَّسُولُ ٱللَّهِۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلۡكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيۡنَهُمۡۖ تَرَىٰهُمۡ رُكَّعٗا سُجَّدٗا يَبۡتَغُونَ فَضۡلٗا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضۡوَٰنٗاۖ سِيمَاهُمۡ فِي وُجُوهِهِم مِّنۡ أَثَرِ ٱلسُّجُودِۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمۡ فِي ٱلتَّوۡرَىٰةِۚ وَمَثَلُهُمۡ فِي ٱلۡإِنجِيلِ كَزَرۡعٍ أَخۡرَجَ

[3]- Surat At-Tawba/100.

شَطْـَٔهُۥ فَـَٔازَرَهُۥ فَٱسْتَغْلَظَ فَٱسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِۦ يُعْجِبُ ٱلزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ ٱلْكُفَّارَ ۗ وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟
وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ مِنْهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًۢا ﴾

"Muhammad ni Mtume wa Allaah, na wale ambao wako pamoja naye ni wakali dhidi ya makafiri na ni wenye kuhurumiana baina yao, utawaona wao hali ya kuwa ni wenye kurukuu na wenye kusujudu wanatafuta fadhila kutoka kwa Allaah na radhi, alama zao zipo katika nyuso zao kutokana na athari ya kusujudu. Hiyo ndio sifa yao iliyo katika Taurat. Na sifa yao katika Injili ni kama mmea uliotoa tawi lake, ukautia nguvu, ukanenepa, na ukasimama sawa juu ya kigogo chake (ukiwa na mandhari nzuri) unaowapendeza wakulima, ili kuwatia hasira makafir. Amewaahidi Allaah walioamini na wakatenda amali njema katika jinsi ya hao Maswahaba msamaha na ujira mkubwa"[4].

Na Allaah Ta'alaa amesema:

﴿ لَّقَدْ رَضِىَ ٱللَّهُ عَنِ ٱلْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ ٱلشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِى قُلُوبِهِمْ فَأَنزَلَ ٱلسَّكِينَةَ
عَلَيْهِمْ وَأَثَٰبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا ﴾

"Hakika amewaridhia Allaah waumini wakati walipokupa kiapo cha utiifu chini ya mti, ameyajuwa Allaah yaliyomo katika nyoyo zao akateremsha utulivu juu yao na akawapa wao ushindi ulio karibu"[5].

Na Allaah Ta'alaa amesema:

﴿ لِلْفُقَرَآءِ ٱلْمُهَٰجِرِينَ ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَٰرِهِمْ وَأَمْوَٰلِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَٰنًا
وَيَنصُرُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلصَّٰدِقُونَ *** وَٱلَّذِينَ تَبَوَّءُو ٱلدَّارَ وَٱلْإِيمَٰنَ مِن قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ
مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِى صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِّمَّآ أُوتُوا۟ وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ
خَصَاصَةٌ ۚ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِۦ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴾

---

[4]- Surat Al-Fat'h/29.

[5]- Surat Al-Fat'h/18.

“Wapewe mali hiyo Mafakiri wa Muhajirina ambao wametolewa katika miji yao na wakaepushwa na mali zao hali ya kuwa wanatafuta fadhila na radhi na hali ya kuwa wanainusuru dini ya Allaah na Mtume wake. Hao ndio Wakweli ** Na wale ambao wamechagua mji wa madina kuwa maskani na Uislamu kuwa ni Imani kabla ya hao Muhajirina, wanawapenda wale waliohamia kwao na wala hawapati katika nyoyo zao husda kwa walichopewa

na wanawapendelea kuliko nafsi zao ijapokuwa upo kwao uhitaji. Na yeyote atakaekingwa na ubakhili wa nafsi yake basi hao ndio wenye kufaulu”[6].

Kama alivyowasifu Mtume -swala na salamu zimshukie- katika hadithi nyingi na kutaja fadhila zao, kama alivyosimulia Ibn Masoud -Allaah amridhe- kutoka kwa Mtume -swala na salamu zimshukie- amesema:

«خَيْرُكُمْ قَرْنِي، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ»

“Wabora wenu ni wale walioishi katika karne yangu, kisha wenye kuwafuatia hao, kisha wenye kuwafuatia hao”[7].

Kadhalika amesimulia Abu Huraira -Allaah amridhie- kwamba Mtume -swala na salamu zimshukie- amesema:

«لَا تَسُبُّوا أَصْحَابِي، لَا تَسُبُّوا أَصْحَابِي، فَوَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ أَنْفَقَ مِثْلَ أُحُدٍ ذَهَبًا، مَا أَدْرَكَ مُدَّ أَحَدِهِمْ، وَلَا نَصِيفَهُ»

“Msiwatusi Maswahaba wangu, msiwatusi Maswahaba wangu. Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, lau mmoja wenu alitoa sadaka ya dhahabu mfano wa jabali Uhud (kwa ukubwa), asingefikia kibaba cha mmoja wao wala nusu yake”[8].

Na amesimulia Abu Huraira -Allaah amridhie- kwamba Mtume -swala na salamu zimshukie- amesema:

---

[6]- Surat Al-Hashri/8-9.
[7]- Bukhari (2651) na Muslim (2535).
[8]- Bukhari (2651) na Muslim (2535).

«النُّجُومُ أَمَنَةٌ لِلسَّمَاءِ، فَإِذَا ذَهَبَتِ النُّجُومُ أَتَى السَّمَاءَ مَا تُوعَدُ، وَأَنَا أَمَنَةٌ لِأَصْحَابِي، فَإِذَا ذَهَبْتُ أَتَى أَصْحَابِي مَا يُوعَدُونَ، وَأَصْحَابِي أَمَنَةٌ لِأُمَّتِي، فَإِذَا ذَهَبَ أَصْحَابِي أَتَى أُمَّتِي مَا يُوعَدُونَ»

"Nyota ni walinzi wa mbingu, ikiwa nyota zikiondoka basi itaijilia mbingu kile alicho ahidiwa (kiama), na mimi ni mlinzi kwa Maswahaba wangu, nikiondoka mimi kitawajilia Maswahaba wangu kile walicho ahidiwa (fitna, vita n.k), na

Maswahaba wangu ni walinzi wa umma wangu, wakiondoka Maswahaba wangu yatawajilia umma wangu yale walio ahidiwa (bidaa na mfarakano n.k)"[9].

Na waislamu wote wamekubaliana juu ya uwajibu wa kuwapenda Maswahaba, kuwaombea dua (kwa kusema): Radhiallaahu 'anhum na kujitenga na wale ambao wanawatusi Maswahaba na kuwatia dosari, na zimekuja kwa hilo kauli nyingi za Salaf, miongoni mwa hizo:

«إِنَّ اللَّهَ نَظَرَ فِي قُلُوبِ الْعِبَادِ، فَوَجَدَ قَلْبَ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ خَيْرَ قُلُوبِ الْعِبَادِ، فَاصْطَفَاهُ لِنَفْسِهِ، فَابْتَعَثَهُ بِرِسَالَتِهِ، ثُمَّ نَظَرَ فِي قُلُوبِ الْعِبَادِ بَعْدَ قَلْبِ مُحَمَّدٍ، فَوَجَدَ قُلُوبَ أَصْحَابِهِ خَيْرَ قُلُوبِ الْعِبَادِ، فَجَعَلَهُمْ وُزَرَاءَ نَبِيِّهِ، يُقَاتِلُونَ عَلَى دِينِهِ»

"Hakika Allaah alitazama nyoyo za waja akaupata moyo wa Muhammad kuwa ndio bora ya mioyo ya waja, akamchagua na akampa utume, kisha akataza mioyo ya waja baada ya moyo Muhammad akaipata mioyo ya Maswahaba wake ndio bora ya mioyo ya waja, akawafanya wao kuwa ni wasaidizi wa Mtume wake, wanaopigana kutetea Dini yake". Tazama: [Musnad Ahmad], (3600).

Na amesema Ibn Omar -Allaah awaridhie- yeye na baba yake -

«لاَ تَسُبُّوا أَصْحَابَ مُحَمَّدٍ صَلَّى الله عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَلَمَقَامُ أَحَدِهِمْ سَاعَةً خَيْرٌ مِنْ عَمَلِ أَحَدِكُمْ عُمْرَهُ»**"Msiwatukane Maswahaba wa Muhammad -swala na salamu zimshukie kusimama mmoja wao (katika jihad au ibada yoyote) kitambo cha saa ni bora kuliko ibada za mmoja wenu umri wake wote"[10].**

---

[9]- Muslim (2531).

[10]- Ameipokea Imam Ahmad katika kitabu [Al-Fadhwaail (Jz. 1, Uk. 57)] na Ibn Abi Shaiba (Jz. 6, Uk. 405) na Ibn Abi 'Aaswim katika kitabu [As Sunnah (Jz. 2, Uk. 484)].

Alikuja mtu mmoja kwa Abdullaahi Bin Mubaarak (aliyefariki mwaka 181h) akamuuliza: Je ni Muawiya ndie bora au Umar Bin Abdil Aziz? Akaema: **"Mchanga uliopo katika tundu za pua ya Muawiya (wakati) akiwa pamoja na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- ni bora kuliko Umar Bin Abdil Aziz"**[11].

Amesema Abu Zur'a -Allaah amrehemu- (aliyefariki mwaka 264h): **"Ukimuona mtu anamvunjia heshima mmoja katika Maswahaba wa Mtume -swala na salamu zimshukie- basi juwa kwamba huyo ni mzandiki, na hilo ni kwa sababu Mtume ni wa haki na Qur'an ni haki, na hakika wametufikishia sisi hii Qur'an na Sunnah Maswahaba wa Mtume -swala na salamu zimshukie-, na hakika si vingine (hao wanaovunja heshima) wanakusudia kuwakosoa mashahidi wetu ili wapate kukibatilisha kitabu chetu na sunnah, basi kuwakosoa wao ndio bora na hao ni wazandiki"**[12].

Na amesema Imamu Twahawi -Allaah amrehemu- (aliyefariki mwaka 321h): **"Na tunawependa Maswahaba wa Mtume -swala na salamu zimshukie- wala hatuvuki mipaka katika kumpenda yeyote miongoni mwao, na wala hatujitengi na yeyote miongoni mwao na tunamchukia yule anayewachukia na kuwataja (kwa ubaya) pasi na haki, na wala hatuwataji wao isipokuwa kwa kheri, na kuwapenda wao ni Dini, Imani na Ihsani, na kuwachukia wao ni Ukafiri, Unafiki na Uovu"**[13].

Na amesema Ibn Sswalaah -Allaah amrehemu- (aliyefariki mwaka 643h): **"Hakika umma wote umekubaliana juu ya kuwafanya waadilifu Maswahaba wote, hata yule ambaye ilitokea fitna miongoni mwao, na wamekubaliana kadhalika maulamaa wote ambao Ijmaa (makubaliano) yao yanazingatiwa"**[14].

---

[11]- Ameipokea Ibn Asaakir (Jz. 59, Uk. 208).
[12]- Al-Kifaaya (Uk. 97) cha Al-Khatib na Tareikh Dimashki (Jz. 37, Uk. 132).
[13]- Tazama kitabu: [Al-Aqidat Twahaawiyyah].
[14]- Tazama Kitabu: [Muqaddimat Ibn Sswalaah (Uk. 428)].

Amesema Ibn Taymiyyah -Allaah amrehemu- katika kubainisha itikadi ya Ahlus Sunnah kuhusiana na Maswahaba: "… **Na wanajizuia kutaja magomvi yaliyotokea baina yao, na wanasema athari zilizopokewa katika mabaya yao kuna miongoni mwa hizo ni uwongo, na kuna zilizo zidishwa ndani yake, kupunguzwa, na kubadilishwa kinyume na ukweli wake, na iliyo sawa katika hili (ni kusema): wao katika hilo ni wenye kupewa udhuru, ima wajejitahidi na wakapatia au wamejitahidi na wakakosea…, na wana wao fadhila nyingi na (kheri nyingi) zilizotangulia ambazo ni sababu ya kusamehewa yale yaliyojiri baina yao, kiasi ambacho husamehewa wao madhambi tafauti na wale waliokuja baada yao, kwa sababu wao wametenda mema ambayo yanafuta madhambi yao, jambo ambalo halipatikani kwa waliokuja baada yao, kisha kiwango cha makosa yaliyofanywa na baadhi yao ambayo yanakosolewa ni machache sana kulinganisha na mema yao na uzuri wa Imani yao katika kumuamini Allaah na Mtume wake -swala na salamu zimshukie-, na jihadi waliopigana katika njia ya Allaah, (kadhaalika) hijra, elimu yenye manufaa, bali yeyote mwenye kufuatilia historia yao na fadhila mbalimbali alizowapa Allaah hakika atafahamu kwamba wao ndio viumbe bora baada ya Manabii, hawakuwepo wala hawatakuwepo (watu wengine) mfano wao, na kwamba wao ni watakasifu miongoni mwa watu wa karne zote za umma huu ulio bora na mtukufu mbele ya Allaah"**[15].

NUKTA YA PILI:
NAFASI YA ABUBAKAR SWIDDIIQ ﷺ KHALIFA WA MTUME ﷺ

Wamekubaliana Ahlus Sunnah wal-Jamaa'h wote juu ya kwamba mtu bora katika umma huu baada ya Manabii ni khalifa aliye mbora Abubakar Swiddiiq, kwa kuzingatia riwaya mbalimbli zilizokuja kwa wingi katika kubainisha fadhila zake na cheo chake na tutazitaja riwaya hizo katika risala yetu hii Bi-idhbillaahi.

JINA LAKE: Abdullahi Bin Uthman Bin 'Aamir Bin 'Amri Bin Ka'bi Bin Sa'd Bin Taimi Bin Murra Bin Ka'b Bin Luayyi Bin Ghaalib Al-Kurashi Attaimiy,

[15]- Tazama kitabu: [Al-'Aqiidul waasitiyyah].

inakusanyika nasaba yake pamoja na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kwa Murra Bin Ka'b.
Na mama yake ni: Ummul Khayr, Salma Bint Swakhri Bin 'Aamir Bin 'Amri Bin Ka'bi Bin Sa'd Bin Taimi Bin Murra, ambaye ni bint wa Ammi wa baba yake[16].

Ameitwa kwa Laqab (jina la kubandika) la Swiddiiq kwa sababu ya kutangulia kwake kwenye kumsadikisha Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kama alivyopokea Imam Abu Abdillaahi Al-Hakim -Allaah amrehemu- kwa sanadi yake mpaka kwa Aisha amesema: **"Wakati Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alivyopelekwa usiku masjid Al-aqswa (Palestina), akaamka asubuhi hali ya kuwa anawasimulia (watu) jambo hilo, wakaritadi watu ambao walikuwa wamemuamini na kumsadikisha, kisha wakatoka kwenda kwa Abubakar -Swala na Salamu zimshukie-** wakasema: **(Je utamuamini rafiki yako ambaye anadai kwamba amepelekwa katika sehehemu ndogo ya usiku kwenda Baytul maqdis na akarudi kabla ya kupambauka asubuhi,** akasema: **"Ndio, mimi nitamuamini kwa (kuniambia ameenda) sehemu ya mbali zaidi ya hapo, nitamuamini kwa (kuniambia) habari za mbinguni, (hata) kwa kitambo kidogo cha asubuhi (kwamba alikwenda wakati wa alfajiri na akarudi kabla ya kuchomoa jua), kwa sababu hiyo akaitwa Abubakar As Swiddiiq"[17].**

FADHILA ZAKE NA SIFA ZAKE (ABUBAKAR SWIDDIIQ) :

Fadhila zake ni nyingi sana, kwanza amekuwa pamoja na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kabla ya kupewa utume, pia ni mtu wa mwanzo kumuamini na aliendelea kusuhubiana naye muda wake wote aliokaa Makka, kisha alifuatana nae wakati wa kuhama kwenda Madina na walijificha pamoja pangoni, na alishirikiana nae pia katika vita mbalimbali.

---

[16]- Tazama kitabu: [At-Twabaqaatul Kubra (Jz. 3, Uk. 169)], [As Siiratu Nnabawiyyah] (Jz. 1, Uk. 24) cha Ibn Hishaam, [Al Iswwaba] (Jz. 2, Uk. 333-335), [Fat-hul Baari] (Jz. 7 Uk. 8), [Swifatu Sswaf-wa] (Jz. 1, Uk. 235), na [Hilyatul Auliyaa] (Jz. 1, Uk. 28).

[17] [Al-Mustadraq (Jz. 3, Uk. 62).

Na katika vita vya Tabuk yeye ndiye alikuwa mshika bendera, pia katika mwaka wa tisa aliwaongoza watu kwenye ibada ya Hija hali ya kuwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- yupo hai, na baada ya kufariki Mtume -Swala na Salamu zimshukie- yeye ndiye alikuwa Khalifa (kiongozi) wa waislamu wote, watu wakamuita kwa jina la khalifa wa Mtume ﷺ[18].

FADHILA ZA ABUBAKAR -Allaah amridhie- NDANI YA QUR'AN:

Miongoni mwa dalili zilizokuja kueleza fadhila zake ndani ya Qur'an ni:

1. **Dalili ya kwanza**:

﴿إِلَّا تَنصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ ٱللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ ثَانِىَ ٱثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِى ٱلْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَٰحِبِهِۦ لَا تَحْزَنْ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَنَا ۖ﴾

"Na msipomtetea (Mtume ﷺ), basi Allaah alikwisha mnusuru siku ile Makafiri wa Kikureishi walipomtoa (kwenye mji wake wa Makka), naye ni wa pili kati ya wawili, wakati walipokuwa katika pango, naye akamwambia sahiba wake: Usihuzinike. Hakika Allaah yu pamoja nasi"[19].

Wamekubaliana waislamu wote kwamba makusudio ya neno [Swaahib- **الصَّاحِبُ**] katika aya hii ni Abubakri Sidiiq رضي الله عنه[20].

Amesema Sufyan At-Thauri -Allaah amrehemu-: **"Allaah amewalaumu waislamu wote kuhusu (kumnusuru Mtume ﷺ), isipokuwa Abubakar رضي الله عنه peke yake, yeye ametolewa katika lawama"[21]**. Kisha akaisoma aya iliyotangulia.

Amesema Ibn Jarir -Allaah amrehemu-: **"Allaah aliposema: [Wa pili katika wawili] anakusudia Mtume ﷺ na Abubakri رضي الله عنه, kwa sababu wao wawili ndio waliotoka hali ya kuwakimbia Makureishi pindi walipokusudia kumuuwa Mtume**

---

[18]- Tazama: [Al-iswaaba] (Jz. 2, Uk. 333), [A'laamu Nnubuwwat] cha Al-Maawardi (284-285) na [Tahdhiibul asmaai wal-lughaat] (Jz. 2, Uk. 184).
[19]- Surat Ttauba/40.
[20]- Tazama: [Al-iswaaba] (Jz. 2, Uk. 335), [Taareikhul khulafaa] cha Suyutwi, (Uk. 48), [Tuhfatul ahwadh] (Jz. 10, Uk. 154) na [Sharhu kitaabil fiqhil akbar] cha Mulaa Aliy Al-Qaari (Uk. 101).
[21]- Tazama: [As sharii'ah] (Jz. 4, Uk. 1823).

ﷺ kisha wakajificha ndani ya pango. Na aliposema: [Wakati walipokuwa katika pango], anasema: Wakati Mtume ﷺ na Abubakar ﷺ naye Mtume ﷺ akamwambia swahiba wake: [Usihuzunike], kwa sababu yeye Abubakar ﷺ alipata wasiwasi kwa (Makureish) waliokuwa wanaowatafuta, wasije wakajuwa sehemu yao waliojificha, akapata woga kutokana na hilo, ndio Mtume ﷺ akamwambia:

[Usihuzunike. Hakika Allaah yu pamoja nasi], atatunusuru, washirikina hawatajuwa mahali tulipo wala hawatatufikia"[22].

Na amesema Al-Haafidh Ibn Kathir -Allaah amrehemu-:

﴿إِذۡ أَخۡرَجَهُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ ثَانِيَ ٱثۡنَيۡنِ﴾

"Walipomtoa (kwenye mji wake wa Makka), naye ni wa pili kati ya wawili".

"Katika mwaka wa Hijra (mwaka aliohama), wakati washirikina walipokusudia kumuuwa, kumfunga (jela) au kufukuzwa (mji wa Makka), Mtume ﷺ akatoka hali ya kuwakimbia wao (makafiri), akiwa amesuhubiana na rafiki yake Abubakar Ibn Abi Quhafa ﷺ, wakajificha siku tatu ndani ya pango la Jabal thauri, ili wapate kurudi watu ambao walitoka nyuma yao kuwafuatilia, kisha waendelee na safari yao kuelekea Madina, (wakiwa ndani ya pango) Abubakri akaanza kupata wasiwasi asije mmoja wao akawaona, akawa anamkinga Mtume ﷺ kutokana na maudhi yao, lakini Mtume ﷺ akawa anamtuliza na kumthibitisha hali ya kuwa anasema: [Ewe Abubakar, ni ipi dhana yako kwa watu wawili Allaah ni wa-tatu wao?]. [Bukhari] (4663) na [Muslim] (2381).

Ndio maana Allaah Ta'aala akateremsha utulivu katika nyoyo zao:

﴿فَأَنزَلَ ٱللَّهُ سَكِينَتَهُۥ عَلَيۡهِ﴾

"Allaah akateremsha utulivu wake kwenye moyo wa (Mtume) wake"[23].

---

[22]- Tazama kitabu: [Jaamiul Bayaan] (Jz. 14, Uk. 257-258).

[23]- Surat Ttauba/40

Na katika kauli maarufu ni (kwamba aliteremsha utulivu wake) juu ya Mtume ﷺ na imesemwa kuwa ni Abubakri رضي الله عنه"[24].

Na Imamu Abubakar Ibnul 'Arabi -Allaah amrehemu-, baada ya kauli ya Mtume ﷺ: **[Ewe Abubakar, ni ipi dhana yako kwa watu wawili Allaah ni wa-tatu wao?].**

Amesema (Ibnul Arabi -Allaah amrehemu-): **"Hii ni fadhila kubwa na daraja ya juu, haiwezekani kwa mtu yeyote kuelezea kwamba Allaah ni wa-tatu katika wawili, mmoja wao ni Abubakar رضي الله عنه, kama vile (Allaah) alivyomtaja Mtume ﷺ na Abubakar رضي الله عنه: [ni wa pili katika wawili]".** **[Ahkaamul Qur'an] (Jz. 2, Uk. 951).**

Amesema Nasir Bin Ali As-Sheikh -Allaah amhifadhi-: **"Aya hii ni ushahidi wa wazi juu ya fadhila za Abubakri رضي الله عنه, pale Allaah alipomfanya kuwa ni wa pili kwa Mtume ﷺ kwa kauli yake: [naye ni wa pili kati ya wawili (yeye na Abubakar Siddiiq), wakati walipokuwa katika pango]. Halikuwa hilo ila ni kwa sababu Abubakar Siddiiq رضي الله عنه amefikia ukomo katika fadhila"**[25].

2. **<u>Dalili ya Pili</u>:**

Amesema Allaah Ta'ala:

﴿وَٱلَّذِى جَآءَ بِٱلصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِۦٓ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُتَّقُونَ﴾

"Na yule aliyekuja na ukweli na akaukubali (kiimani na vitendo), hao ndio wenye kumcha Allaah"[26].

Amepokea Imam Ibn Jarir -Allaah amridhie- kwa sanadi yake mpaka kwa Ally Bin Abi Twalib رضي الله عنه kuhusu kauli yake (Allaah): **[Na yule aliyekuja na ukweli],** amesema: (hapo anakusudiwa Mtume) Muhammad ﷺ **[Na akaukubali (kiimani na vitendo)].** (hapo anakusudiwa) Abubakar رضي الله عنه[27].

---

[24]- Tazama: [Tafsiiru Ibn Kathir] (Jz. 3, Uk. 402).
[25]- Tazama: ['Aqiidat Ahlis Sunnah fis Swahabatil kiraam]. Nassor Aliy As-Sheikh (Jz. 1, Uk. 221).
[26]- Tazama: [Surat Az-Zumar/33].
[27]- Tazama: [Jaamiul bayaan] (Jz. 24, Uk. 3) na [Ad-Durrul manthuur] (Jz. 7, Uk. 228).

3. **Dalili ya Tatu:**

Kauli yake Allaah:

﴿وَإِن تَظَٰهَرَا عَلَيۡهِ فَإِنَّ ٱللَّهَ هُوَ مَوۡلَىٰهُ وَجِبۡرِيلُ وَصَٰلِحُ ٱلۡمُؤۡمِنِينَۖ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ بَعۡدَ ذَٰلِكَ ظَهِيرٌ﴾

"Na kama mkisaidiana dhidi yake (kufanya yanayomuudhi), hakika Allaah ndiye mwenye kumnusuru na Jibril na walio wema katika Waumini. Na Malaika, baada hayo yote niwasaidizi"[28].

Maulamaa wengi wa tafsiri wanasema kwamba maana ya: **[na walio wema katika Waumini],** makusudio yake ni Abubakar na Umar Allaah awaridhie[29].

4. **Dalili ya Nne:**

Amesema Allaah Ta'ala:

﴿ فَأَمَّا مَنۡ أَعۡطَىٰ وَٱتَّقَىٰ ** وَصَدَّقَ بِٱلۡحُسۡنَىٰ ** فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلۡيُسۡرَىٰ﴾

"Basi mwenye kutoa na akamcha Allaah ** Na akalisadikisha neno jema ** Basi tutamsahilishia yeye lililo jepesi"[30].

Amesema Ibn Abi Haatim -Allaah amrehemu-: **"Imepokewa kutoka Zaid Bin Aslam amesema: (maana ya aya hii): [Tutamsahilishia yeye lililo jepesi] ni pepo"[31].**

Amesema Imam Ibn Jarir Ttwabari -Allaah amridhie-: **"Na imesemwa kwamba aya hii imeteremka kwa Abubakar Siddiq رضي الله عنه"[32].**

Hizi ni baadhi ya aya katika Qur'an zinzaojulisha kwamba Abubakar رضي الله عنه ni mbora wa viumbe baada ya Manabii -Alaihimus swalaatu was salaam-.

---

[28]- Tazama: [Surat At-Tahrim/4].

[29]- Tazama kitabu: [Jaamiul 'uluumi] (Jz. 28, Uk. 162-163), [Al-Jaami'ul liahkaamil Qur'an] (Jz. 18, Uk. 192), [Tafsir Ibn Kathir] (Jz. 7, Uk. 56) na [Ad-Durrul manthuur] (Jz. 8, Uk. 223-224).

[30]- Tazama: [Surat Al-Lail/5-7].

[31]- Tazama kitabu: [Tafsir Ibn Abi Haatim] (Jz. 10, Uk. 3441).

[32]- Tazama kitabu: [Tafsiru Ttwabari] (Jz. 24, Uk. 465).

BAADHI YA HADITHI ZINAZOELEZEA FADHILA ZA ABUBAKRI ﷺ

1) Amesema Abubakar Siddiiq ﷺ

"Nilitazama kwenye miguu ya washirikina juu ya vichwa vyetu, hali yakuwa sisi tuko pangoni, nikasema: Ewe Mtume wa Allaah, lau mmoja wao atatazama miguu yake atatuona, akasema: [Ewe Abubakar, ni ipi dhana yako kwa watu wawili Allaah ni watatu wao?]"[33].

Amesema Imam Nnawawi -Allaah amrehemu-: **"Kuna katika hadithi hii fadhila za Abubakar ﷺ nazo ni miongoni mwa sifa zake tukufu, na fadhila zake ni nyingi, miongoni mwake ni hadithi hii, na miongoni mwa fadhila zake ni kujitoa nafsi yake, kuachana na watu wake pia mali yake, kuongozana kwake katika kumtii Allaah Ta'alaa na Mtume ﷺ wake, kulazimiana kwake na Mtume ﷺ na kupingana na watu katika (kumnusuru Mtume), na miongoni mwa fadhila hizo ni kuijaalia kwake kuwa ni ngao ya kumkinga yeye (Mtume ﷺ) na mengine yasiyokuwa hayo"[34].**

2) Amesema Mtume ﷺ :

"Hakika katika watu wenye kujitoa zaidi kwangu katika usuhuba/urafiki wake na mali yake ni Abubakar ﷺ, lau ningelikuwa ni mwenye kujifanyia mimi mwandani (rafiki kipenzi) asiyekuwa Mola wangu Mlezi, basi ningemfanya Abubakar (mwandani), lakini (utabaki) udugu wa kiislamu na kupendana"[35].

Amesema Imam Nnawawi -Allaah amrehemu-: **"Wamesema Maulamaa: maana yake ni (kwamba Abubakar) ni mwingi zaidi kwa kutoa na mwepesi kwetu sisi kwa nafsi na mali yake, na huku si kusimbulia kwa kuhesabu (mema) uliyofanya, kwa sababu huo ni udhia (na ni jambo) lenye kubatilisha thawabu, na kwa sababu (mwenye haki ya kuhesabu na kusimbulia) ni Allaah na Mtume wake -swala na salamu zimshukie-"[36].**

---

[33]- Tazama kitabu: [Bukhari] (4663) na [Muslim] (2381).
[34]- Tazama kitabu: [Sharhu Muslim] (Jz. 15, Uk. 150).
[35]- Tazama kitabu: [Bukhari] (3904).
[36]- Tazama kitabu: [Sharhi Muslim] (Jz. 15, Uk. 150). [Fat-hul baari] (Jz. 1, Uk. 559).

Na amesema Imamu Al-Qurtubi -Allaah amrehemu-: **"Makusudio ni kwamba Abubakar ana haki ambazo lau (mtu) mwingine angekuwa nazo mfano wake basi angesimbulia (angejifakharisha) nazo, hilo linaungwa mkono na kauli yake katika riwaya ya Ibn Abbas -Allaah amridhie- [Hakuna yeyote mwenye (haki ya) kunisimbulia katika mali yake na nafsi yake zaidi ya Abubakar Ibn Abi Quhafa]**[37]**.** Wallaahu 'alam.

3) Pia Mtume ﷺ amesema:

«لَا تُبْقَيَنَّ فِي الْمَسْجِدِ خَوْخَةٌ إِلَّا خَوْخَةَ أَبِي بَكْرٍ»

"Usiachwe katika msikiti huu mlango wowote (milango yote izibwe) isipokuwa mlango wa Abubakri ﷺ "[38]**.**

Amesema Imamu Nnawawi -Allaah amrehemu-: **"Neno (خَوْخَة - Khaukha) kwa kutiwa fat-ha herufi ya Khaa, maana yake ni mlango mdogo uliopo baina ya nyumba mbili na mfano wake, na katika hadithi hii kuna fadhila na kipaumbele cha wazi kwa Abubakar ﷺ".**

4) Imamu Muslim -Allaah amrehemu- ameitaja hadithi katika sahihi yake kwamba mwanamke mmoja alikuja kwa Mtume ﷺ, akamuamrisha arudi kesho (siku ya pili), akauliza:

أَرَأَيْتَ إِنْ جِئْتُ وَلَمْ أَجِدْكَ؟ كَأَنَّهَا تَقُولُ: المَوْتَ، قَالَ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «إِنْ لَمْ تَجِدِينِي فَأْتِي أَبَا بَكْرٍ»

"Unaonaje nikija na sijakukuta?, kana kwamba yeye anakusudia: (akiwa) umekufa, akasema Mtume ﷺ : [Kama hukunikuta basi nenda kwa Abubakar]"[39]**.**

5) Imepokewa kutoka kwa Aisha -Allaah amridhie- kwamba Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesema:

---

[37]- Tazama kitabu: [Bukhari] (467).

[38]- Tazama kitabu: [Sahihi Muslim] (2382).

[39]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari] (2386).

"ادْعِي لِي أَبَا بَكْرٍ، أَبَاكِ، وَأَخَاكِ، حَتَّى أَكْتُبَ كِتَابًا، فَإِنِّي أَخَافُ أَنْ يَتَمَنَّى مُتَمَنٍّ وَيَقُولُ قَائِلٌ: أَنَا أَوْلَى، وَيَأْبَى اللهُ وَالْمُؤْمِنُونَ إِلَّا أَبَا بَكْرٍ"

"Niitie mimi baba yako Abubakar na ndugu yako, ili niandikie barua, kwa sababu mimi nachelea (asije) akatamani mwenye kutamani na akasema mwenye kusema: mimi ndiye bora (mwenye kustahiki ukhalifa) na Allaah pamoja waumini hawakubali isipokuwa (awe) Abubakar"[40].

6) Na imekuja katika Musnad Ahmad, Tirmidh na Twahawiyya kutoka kwa Hudhaifa kwamba Mtume Swala na Salamu zimshukie amesema:

"اقْتَدُوا بِاللَّذَيْنِ مِنْ بَعْدِي أَبِي بَكْرٍ، وَعُمَرَ"

"Wafuateni wale wawili baada yangu Abubakar na Omar"[41].

7) Ametaja Imamu Bukhari na Muslim katika sahihi zao kutoka kwa Abu Musa -Allaah amridhie- amesema: **"Mtume ﷺ aliugua na yalipozidi maradhi yake alisema: [Muamrisheni Abubakar awaswalishe watu]. Akasema Aisha: Hakika yeye ni mtu (mwenye moyo) laini, hawezi kusimama mahala pako kuwaswalisha watu. Akasema (Mtume ﷺ): [Muamrisheni Abubakar awaswalishe watu]. (Aisha) akarudia tena (maneno yake). Akasema (Mtume ﷺ): [Muamrishe Abubakar awaswalishe watu, hakika nyinyi ni (sawa) wanawake (katika zama za Nabii) Yusuf]. Kisha Mtume ﷺ akamwendea (Abubakar), na yeye akawaswalisha watu katika uhai wa Mtume ﷺ"[42].**

Amesema Imamu Suyutwi -Allaah amrehemu-: **"Wamesema Maulamaa: kuna katika hadithi hii dalili ya wazi juu ya kwamba (Abubakar) Swiddiiq ndiye swahaba mbora zaidi kuliko wote, na ndiye Mwenye haki zaidi kwao kwa Ukhalifa na Mwenye kustahiki zaidi Kuongoza"[43].**

8) Ametaja Imamu Bukhari na Muslim katika sahihi zao kwamba Mtume ﷺ alimchagua Abubakar Siddiiq -Allaah amridhie- kuwa khalifa wake katika

---

[40]- Tazama kitabu: [Bukhari] (5666) na [Muslim] (2387).
[41]- Tazama kitabu: [Musnad Ahmad] (23245), [Tirmidh] (3662) na [Musnad Al-Bazzaar] (2827).
[42]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari] (678) na [Muslim] (420).
[43]- Tazama kitabu: [Taareikhul Khulafaa], (Uk. 63).

kuongoza (ibada ya) Hija mwaka wa tisa hijria, ili apate kuwaongoza waislamu katika Hija yao[44].

Amesema Ibn Taymiyyah -Allaah amrehemu-: **"Hakika ni jambo lenye kujulikana kwamba mbele ya wanachuoni wa Tafsiri, Sera, Hadithi na Fiqh na wengine, kwamba Mtume ﷺ alimchagua Abubakar Siddiq mwaka wa tisa kuwa kiongozi wa Hija, na hiyo ndiyo Hija ya kwanza kupatikana katika Uislamu kutokea (mji wa) Mtume ﷺ Madina, wala haikupatikana kabla ya hapo Hija yoyote katika Uislamu isipokuwa Hija ambayo aliongoza 'Itaab Bin Useid Bin Abil 'Aas Bin Umayyah kwa watu wa Makka mwaka wa nane, aliyechaguliwa na Mtume ﷺ kuwaongoza watu wa Makka katika mwaka huo ambao ulikombolewa mji wa Makka, kisha katika mwaka wa tisa baada ya Mtume kurudi katika vita vya Tabuk alimchagua Abubakar -Allaah amridhie- kuongoza msafara wa Hija na pia alimuamrisha kutoa tangazo ya kwamba:**

"أَنْ لَا يَحُجَّ بَعْدَ الْعَامِ مُشْرِكٌ، وَلَا يَطُوفَ بِالْبَيْتِ عُرْيَانٌ"

"Asihiji baada ya mwaka huu mshirikina yeyote, wala asitufu Al-Ka'ba aliye uchi".

Na wala Mtume ﷺ hakuwahi kumuamrisha yeyote kutawalia mfano wa jambo hili isipokuwa Abubakar, kwa hiyo katika hili kuna fadhila maalumu kwake, kama vile ambavyo hakuwahi kumtanguliza mtu yeyote kuwaswalisha watu isipokuwa Abubakar -Allaah amridhie- na Hija hii Ally (Bin Abi Twalib) alikuwa ni miongoni mwa wafuasi wake, na wakati (Abubakar) alipokutana na (Ally) alimuuliza: [Je wewe ni kiongozi au raia (wa kawaida)?] Ally akajibu: [Bali mimi ni raia (si kiongozi)], na alikuwa akiswali nyuma ya Abubakar pamoja na waislamu wengine na pia alikuwa akimtii amri yake sawa na watu wengine"[45].

9) Na amepokea Bukhari na Muslim Hadithi ya Abu Huraira -Allaah amridhie- kwamba Mtume -Swala na Salamu zimshukie- aliswalisha swala ya asubuhi, kisha akawaelekea watu akasema:

---

[44]- Tazama: Bukhari (4105) na Muslim (1347).

[45]- Tazama: [Minhaaju Ssunnah] (Jz. 5, Uk. 90).

"Wakati mtu mmoja (katika Bani Israil) alipokuwa anachunga ng'ombe alimpanda na akaanza kumpiga, akasema (yule ng'ombe): Hakika sisi hatukuumbwa kwa ajili ya kazi hii, sisi tumeumbwa kwa ajili ya kulima. Watu wakasema (kwa mshangao): Subhaanallaah (kutakasika na makosa ni kwa Allaah, ng'ombe anaongea! (Mtume akasema): "Mimi, Abubakar na Omar tunaamini haya", (na hali ya kuwa Abubakar na Omar hawakuwepo mahala hapo). Na wakati mtu mmoja alipokuwa anachunga wanyama wake, punde aliwavamia mbwa mwitu, akaondoka na mbuzi mmoja, akamtafuta mpaka alipomnyakua (mbuzi wake) kutoka kwa mbwa mwitu huyo, akasema: leo umemuokoa kutoka kwangu, basi, nani ataemuokoa siku itakapotokea fitna (watu watakapowakimbia wanyama wao), siku atakapokosa mchungaji (na) mimi (nikaweza kumuwinda kwa wepesi)?, watu wakasema: Subhaanallaah, mbwa mwitu anaongea! akasema: mimi naamini (hivyo), pia Abubakar na Omar wanaamini"[46].

Huu ni ushahidi wa wazi kutoka kwa yule ambaye hatamki kwa matamanio ya nafsi yake juu ya kuthibitisha ukamilifu wa Imani ya Maswahaba hawa wawili (Abubakar na Omar -Allaah awaridhie-) na kwamba wao wanakiamini kila kilichothibiti katika Uislamu bila upinzani wowote.

MAKUBALIANO (IJMAA) YA MAULAMAA WOTE JUU YA UBORA WA ABUBAKAR KULIKO MASWAHABA WOTE

Amesema Imam Nnawawi -Allaah amrehemu-: **"Wamekubaliana Ahlus sunnah juu ya kwamba swahaba mbora kuliko wote ni Abubakar kisha Omar"[47].**

Amesema Imam Qustwallaani -Allaah amrehemu-: **"Wamekubaliana Ahlus Sunnah kwamba (swahaba) aliye mbora kuliko wote ni Abubakar kisha Omar"[48].**

Na amesema Imam Qustwallaani -Allaah amrehemu-: **"Mbora wa Maswahaba, bali mbora wa viumbe wote baada ya Manabii -Alaihimus Salaam-**

---

[46]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari], (2324).
[47]- Tazama: [Sharhi Sahihi Muslim] (Jz. 15, Uk. 48).
[48]- Tazama kitabu: [Al-Mawaahibu Lladuniyyah] (Jz. 7, Uk. 36-39).

ni Abubakar kisha baada yake ni Omar Ibnul Khatwaab, kisha Uthman Bin 'Affaan, kisha Ally Bin Abi Twalib". **Tazama: [Al-Baa'ithul athiith] (Uk. 183).**

Na amesema Imam Qustwallaani -Allaah amrehemu-: **"Mbora wao kuliko wote ni Abubakar kisha Omar"[49].**

CHEO CHA AMIIRUL MUMINIIN OMAR IBNUL KHATTWAAB -Allaah amridhie-

JINA LAKE: Anaitwa Omar Ibnul Khattwaab Bin Nufail Bin Abdil 'Uzzaa Bin Riyaah Bin Abdillaahi Bin Qurtwi Bin Razaah Bin 'Adiy Bin Ka'b Bin Luayyi[50] Bin Ghaalib Al-Qurashiy Al-'Adawiy[51]. Inakutana nasabu yake na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kwa Ka'b Bin Luayyi Bin Ghaalib. Kun-ya yake ni Abu Hafsi na Laqab yake ni Al-Farouk, kwa sababu ya juhudi aliyoitoa mpaka Uislamu ukadhihiri katika mji wa Makka na Allaah akafarikisha baina ya Ukafiri na Imani kupitia yeye[52].

Ama baba yake ni Khattwaab Bin Nufail, alikuwa babu yake mzee Naufal Bin Abdil 'Uzza ni mtu ambaye Makureish huenda kwake kwa ajili ya kuhukumiana kesi zao[53]. Ama mama yake ni Hantama Bint Hashim Bin Mughira mtu wa kabila la Makhzuum[54].

DARAJA NA FADHILA ZAKE:

Hakika amuhusihwa Omar -Allaah amridhie- kwa fadhila nyingi tafauti na Maswahaba wengine, fadhila ambazo zimebainisha wazi uwezo wake wa kuongoza umma huu, ndio maana waislamu wote walikubaliana juu ya kuwa yeye ni khalifa baada ya kufariki Abubakar -Allaah amrdhie-.

Amesema Abdullaahi Bin Masoud -Allaah amridhie-: **"Kulikuwa kusilimu kwa Omar ni ukombozi, na Hijra (kuhama) kwake ni ushindi, na Uongozi wake**

---

[49]- Tazama kitabu: [Muqaddimatu Ibni Sswalaah] (Uk. 298).
[50]- Tazama kitabu: [At Twabaqaatul Kubraa] (Jz. 3, Uk. 265). Cha Ibn Sa'd na kitabu: [Mahdhwu Sswawaab] (Jz. 1, Uk. 131). Cha Ibn Abdil Haadi.
[51]- Tazama kitabu: [Mahdhwu Sswawaab] (Jz. 1, Uk. 131). Cha Ibn Abdil Haadi.
[52]- Tazama kitabu: [Sahihi Ttauthiiq fii siirat wahayaatil Farouq Omar Ibnil Kattwaab. (Uk. 15).
[53]- Tazama kitabu: [Nasabu Qureish] (Uk. 347). Cha Az-Zubeiri.
[54]- Tazama kitabu: [Tareikhu Ttwabari] (Jz. 2, Uk. 561) na [Mustadrakul Haakim] (Jz. 1, Uk. 8081)

ni rehma, hakika tulikuwa sisi hatuwezi kuswali Baitil haram (Makka) mpaka aliposilimu Omar, zamani aliposilimu Omar aliwapiga (vita) wao mpaka wakatuacha hatimaye tukaweza kuswali (katika msikiti huo)"[55].

Na amesema Abdullaahi Bin Abbaas -Allaah amridhie-: **"Mtu wa mwanzo kudhihirisha Uislamu ni Omar Ibnul Khattwaab"[56].**

Na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- aliwahi kumuombea dua (Omar) kwamba Allaah autie nguvu Uislamu kwa kusilimu kwake na ikajibiwa dua yake, kama alivyosimulia Ibn Omar kwamba Mtume amesema: **"Ewe Allaah Utie nguvu Uislamu kwa anaependeza zaidi katika watu hawa wawili Abu Jahli au Omar Ibnil Khattwaab".** Amesema (Ibn Omar): **"Na alikuwa anaependeza zaidi kwake ni Omar"[57].**

Na Imam Bukhari ameitaja hadithi ya Jabir Bin Abdillaahi -Allaah amridhie- amesema: Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesema (akimsimulia Omar): **"(Nikiwa katika ndoto) nilijikuta mimi niko peponi, punde nikamuona Rumayswaa mke wa Abu Twalha (Ummu Suleim mamake Anas Bin Malik), kisha nikasikia michakato ya miguu, nikauliza, ni nani huyo? Akasema (Jibril): Huyo ni Bilal. Kisha nikaona nyumba ya kifahari na pembezoni mwake kuna mjakazi, nikauliza. Ni ya nani nyumba hii? Akasema: Nyumba hii ni ya Omar, nikatamani kuingia ili nikaiangalie, nikakumbuka wivu wako".** Akasema Omar: **Namtoa fidia baba yangu na mama yangu kwa ajili yako, Ewe Mtume wa Allaah, hivi nikuonee wewe wivu?! (haiwezekani)"[58].**

Na katika riwaya ya Abu Huraira -Allaah amridhie- amesema: **"Wakati tulipokuwa mbele ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie- mara akasema: [Wakati nikiwa usingizini (kwenye ndoto) nilijiona niko peponi, mara nikamuona mwanamke anatawadha pembezoni mwa nyumba ya kifahari, nikasema: Ni ya**

---

[55]- Tazama kitabu: [At Tabaqaatul kubraa] (Jz. 3, Uk. 270).

[56]- Tazama kitabu: [Al-mu'jamul kabiir] namba (10890). Cha Imam Twabaraani na [Majma'u Zzawaaid] (Jz. 9, Uk. 63), kisha akasema: (Ameipokea Imam At-Twabaraani kwa sanadi nzuri).

[57]- Tazama kitabu: [Sunan Tirmidh] (3681) na [Sahihi Ssiira] (Uk. 193). Cha Sheikh Albani.

[58]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukahri], (3679).

nani nyumba hii? Wakasema: ya Omar, nikakumbuka wivu wake, kisha nikaondoka (bila ya kuingia ndani)]. Omar akalia, na akasema: "Hivi nikuonee wewe wivu, Ewe Mtume wa Allaah!"[59].

Hadithi hizi mbili zimekusanya fadhila za wazi kwa Amiiril Mu'miniina Omar Ibnil Khattwaab -Allaah amridhie- pale ambapo Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesimulia kwamba yeye aliiona nyumba ya kifahari huko peponi iliyoandaliwa kwa ajili ya Omar Ibnil Khattwaab, hii ni alama juu ya takrima kubwa atakayoipata na kuwa daraja yake ni ya juu.

Pia amepokea Bukhari na Muslimu hadithi ya Abu Huraira -Allaah amridhie- kwa sanadi yake amesema: Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesema: **"Hakika walikuwepo katika umati zilizopita kabla yenu watu Muhdathuun, basi akiwepo katika umma huu mtu huyo, basi ni Omar"[60].**

Maana ya Muhdathu ni: mtu anaepewa maono (ilhaam). **Na pia imesemwa:** ni mtu ambaye huzungumza katika ulimi wake maneno ya kupatia na ya usawa bila kukusudia. **Na pia imesemwa:** ni mtu ambaye huzungumzishwa na Malaika bila ya kupewa Utume n.k[61].

Amesema Al-Haafidh Ibn Hajar -Allaah amridhie-: **"Amehusishwa Omar kwa kutajwa kwa sababu ya wingi wa yale yaliyomtokea katika zama za Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kutokana na kupatia (katika maneno yake) ambayo iliteremka Qur'an kuafikiana nayo (kuunga mkono maneno ya Omar), na hata baada ya kufa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- yalitokea kwake mambo mengi ambayo yanaafikiana na vile alivyosema"[62].**

---

[59]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari] (3680).
[60]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari] (3469) na [Muslim] (2398).
[61]- Tazama kitabu: [Fat-hul baari] (Jz. 7, Uk. 50).
[62]- Tazama kitabu: [Fat-hul baari] (Jz. 7, Uk. 51).

MAMBO AMBAYO QUR'AN TUKUFU IMEAFIKIANA NA MANENO YA OMAR رَضِيَ اللهُ عَنْهُ

Miongoni mwa mambo yenye kudhihirisha utukufu wake ni kushuka Qur'an kuafikiana na yale aliyosema, na hilo limepatikana katika matukio mengi, huenda Omar akatoa rai yake kwenye jambo fulani, kisha inateremka Qur'an hali ya kuunga mkono rai hiyo.

Imamu Bukhari amepokea hadithi kwa sanadi yake mpaka kwa Anas -Allaah amridhie- amesema: Amesema Omar -Allaah amridhie-: **"Nimeafikiana na Mola wangu Mlezi katika mambo matatu: nilisema: Ewe Mtume wa Allaah: Lau tungeifanya Maqamu Ibrahim (mahala alipokuwa akisimama Ibrahim) pawe ni mahala pa kuswalia, kisha ikateremka aya: [Na pafanyeni mahala alipokuwa akisimama Ibrahim pawe pa kuswalia]**[63].

Na (katika) aya ya Hijabu, nilisema: [Ewe Mtume wa Allaah, lau ungeliwaamrisha wake zako kuvaa Hijabu, kwa sababu wazawazungumzisha wao watu wema na waovu], kisha ikateremka aya ya Hijabu[64].

Na walipokusanyika wakeze Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kumfanyia yeye wivu nikawaambia: [Asaa (huenda) akiwapeni talaka (akiwaacha), Mola wake Mlezi atampa wake wengine badala yenu nyinyi, walio bora kuliko nyinyi]. Ikateremka aya hiyo"[65].

Na kwa tamko la sahihi Muslim amesema: **"Nimeafikiana na Mola wangu Mlezi kuhusu mambo matatu: kuhusu Maqaamu Ibrahim, Aya ya hijabu, na kuhusiana na mateka wa Badri"**[66].

Na kuafikiana kwake kuhusiana na mateka wa vita vya Badri ni kwamba, watu walikuwa wakimshauri Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, wapo waliosema: Ewe Mtume wa Allaah, hakika Allaah amekupeni ushindi, basi waachie. Akasimama Omar -Allaah amridhie- akasema: **[Niache nizikate**

---

[63]- Tazama: [Surat Al-baqara/125].

[64]- Allaah anasema: **"Enyi mlio amini, msiingie nyumba za Mtume ila mpewe ruhusa"**. Al-Ahzaab/53.

[65]- Tazama kitabu: [Sahihil Bukhari] (402).

[66]- Tazama kitabu: [Sahihi Muslim] (2399).

shingo zao]. (Mtume) akapuuza, kisha akasimama Abubakar akasema: **[Rai yangu ni kuwa watoe fidia na uwasamehe]**, Mtume akawakubalia wao fidia na akawasamehe, kisha Allaah akateremsha aya:

﴿مَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَن يَكُونَ لَهُۥٓ أَسۡرَىٰ حَتَّىٰ يُثۡخِنَ فِي ٱلۡأَرۡضِۚ﴾

"Haifai kwa Nabii yeyote kuwa na mateka mpaka awe ameshinda sawasawa"[67].

Mpaka mwisho wa aya ya tatu mbele yake (aya ya 39). Ikawa aya hizo ni zenye kuafikiana na rai ya Omar -Allaah amridhie-[68].

Na amepokea Imam Ahmad na wengine kutoka kwa Omar -Allaah amridhie- amesema: **"Wakati ilipoteremka aya ya kuharamisha ulevi/pombe alisema: [Ewe Allaah, tubainishie sisi kuhusiana na ulevi ubainifu ambao ni tiba] (inayosheleza)". Ikateremka aya hii ambayo ipo katika surat Al-Baqara:**

﴿يَسۡـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلۡخَمۡرِ وَٱلۡمَيۡسِرِۖ قُلۡ فِيهِمَآ إِثۡمٞ كَبِيرٞ﴾

"Wanakuuliza kuhusiana na ulevi na Kamari. Sema: katika hivyo kuna madhambi kubwa"[69].

Amesema: Aliitwa Omar, akasomewa (aya hizo), kisha akasema: [Ewe Allaah tubainishie sisi kuhusiana na ulevi ubainifu ambao (utakuwa) ni tiba]. Ikateremka aya ya Surat An-Nisaa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقۡرَبُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنتُمۡ سُكَٰرَىٰ﴾

"Enyi mlio amini! Msiikurubie swala hali ya kuwa mmelewa"[70].

Akawa mtoa matangazo wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- anasimama na kusema: Asikurubie swala mtu yeyote aliyelewa. Akaitwa Omar, akasomewa aya hizo, akasema: [Ewe Allaah tubainishie sisi kuhusiana na ulevi ubainifu ambao

---

[67]- Tazama: [Suratul Anfaal/67].
[68]- Tazama: [Jaamiul bayaan] cha Twabari (Jz. 10, Uk. 43-44) na [Tafsiir] Ibn Kathir] (Jz. 3, Uk. 345).
[69]- Tazama: [Surat Al-Baqara/219].
[70]- Tazama: [Surat An-Nisaa/43].

(utakuwa) ni tiba]. Ikateremka aya iliyopo katika Suratu Al-Maida, akaitwa Omar, ikasomwa mbele yake, na wakati alipofika katika (maneno):

﴿ فَهَلْ أَنتُم مُّنتَهُونَ ﴾

"Basi acheni/komeni"[71].

Amesema: akasema Omar -Allaah amridhie-: [Tumeacha tumeacha]"[72].

KUPATIKA MAKUBALIANO (IJMAA') JUU YA UKHALIFA WAKE –Allaah amridhie-

Hakika ulikamilika na kupatikana Ukhalifa wa Omar -Allaah amridhie- kwa makubaliano ya Maswahaba wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, na wamekubaliana Ahlus Sunnah Wal-Jamaah wote juu ya kile walichokubaliana juu yake Maswahaba.

Amesema Imamu Nnawawi -Allaah amrehemu- katika kutaja kwake maafikiano ya Maswahaba juu ya kupitisha pendekezo la Abubakar Swiddiiq -Allaah amridhie- la kuchaguliwa khalifa Omar -Allaah amridhie-:

"Walikubaliana wote juu ya uchaguzi wa Abubakar na kutekeleza ahadi yake kwa Omar". Tazama: [Sharhu Muslim], (Jz. 12, Uk. 206).

Na amesema Sheikhul Islaam Ibn Taymiyyah -Allaah amrehemu-:

"Hakika Abubakar alimchagua Omar na waislamu wakaweka kiapo cha utiifu kwake baada ya Abubakar kufariki, akawa kiongozi wakati ilipopatikana kwake nguvu na mamlaka kwa sababu ya kumpa wao bai'a (kiapo cha utiifu)"[73].

Na amesema Abul 'Izzil Hanafi -Allaah amrehemu- : **"Na tunathibitisha Ukhalifa baada ya Abubakar -Allaah amridhie- kwa Omar -Allaah amridhie- na hilo ni kwa sababu ya kupitisha Abubakar (pendekezo) la Ukhalifa kwake na maafikiano ya Waislamu juu yake baada ya kufariki (Abubakar)"[74].**

---

[71]- Tazama: [Suratul Maida/91].
[72]- Tazama kitabu: [Musnad Ahmad] (378) na [Abu Daud] (3670) na TIrmidh (3049).
[73]- Tazama kitabu: [Minhaaju Ssunna], (Jz. 1, Uk. 142).
[74]- Tazama kitabu: [Shrhu Ttwahaawiyya], (Jz. 1, Uk. 476).

NUKTA YA NNE:

DARAJA LA AMIRUL MUUMINIIN ALLY BIN ABI TWALIB -Allaah amridhie-

- **JINA LAKE NA NASABA YAKE:**

Jina lake ni Ally Bin Abi Twalib Bin Abdil Muttwalib Bin Hashim Bin Abdi Manaaf Bin Quswayyi Bin Kilaab Bin Murra Bin Ka'b Bin Luayyi Bin Ghalib Bin Fihri Bin Malik Bin Nnadhwri Bin Kinana Bin Khuzaima Bin Mudrika Bin Ilyaas Bi Mudhwar Bin Nizaar Bin Ma'addi Bin Adnan. Naye (Ally) ni mtoto wa Ami yake Mtume -Swala na Salamu zimshukie-.

Mama yake ni Fatma Bint Asad Bin Hashim Bin Abdi Manaaf Bin Qaswayyi, na inasemekana kwamba yeye ndiye mwanamke wa kwanza wa kabila la Bani Hashim kumzaa mtoto wa kiume mwenye nasaba na kabila hilo (kwa upande wa baba)[(75)].

- **KUN-YA YAKE:**

Kun-ya yake ni Abul Hasan, au Abu Turaab, au Abu Ssibtwain (baba wa wajukuu wawili wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-)[(76)].

- **FADHILA ZAKE:**

Wamekubaliana Ahlus Sunnah wote Salaf na Khalaf (wazamzni na waliokuja baadae), juu ya kwamba Ally Bin Abi Twalib ndiye mtu bora baada ya (watu watatu): Abubakar, Omar na Uthman -Allaah awaridhie-. Na yeye ni mmoja kati ya Maswahaba kumi waliobashiriwa pepo.
Amefariki hali ya kuwa ameridhiwa na Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, na alikuwa ni miongoni mwa Maimamu na Makhalifa wanne waongofu, ambao tumeamrishwa kufuata mwenendo wao, pia ni katika watu wa mwanzo kusilimu, na ni mtoto wa mwanzo kumuamini Mtume.

---

[75]- Tazama: [At-Twabaqaatul Kubraa (Jz. 3, Uk. 19) na [Al-Bidaayat wan-Nihaayat] (Jz. 7, Uk. 223).
[76]- Tazama: [Usdul Ghaaba] (Jz. 4, Uk. 16) na [Al-Bidaayat wan-Nihaayat] (Jz. 7, Uk. 333).

Amekulia chini ya malezi ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na akamuozesha bint yake Fatma -Allaah amridhie-. Alifanya Hijra kuhamia Madina na alishiriki katika vita vya Badri na vita vingine, isipokuwa vita vya Tabuk, kwa sababu Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alimuacha Madina kuwa ni khalifa (msimamizi wa waislamu), pia alishuhudia (Sulhu ya) Hudaibiya[(77)].

Na zimekuja hadithi nyingi sahihi kuelezea fadhila zake, mongoni mwa hizo: Ni hadithi ya 'Aamir Bin Saad Bin Abi Waqqas, kutoka kwa baba yake amaesema: Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alisema kumwambia Ally -Allaah amridhie-: **"Wewe kwangu mimi ni sawa na Harun kwa Musa, isipokuwa hakuna Mtume baada yangu"[(78)].**

Katika hadithi hii kuna fadhila kubwa imetajwa kuhusu Ally -Allaah amridhie- pale Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alipomjaalia kuwa ni sawa na nafasi ya Harun kwa Musa, kuwa ni ndugu yake, na kumuweka khalifa (kiongozi) kwa watu waliobaki Madina, (wanawake, watoto na watu wenye nyudhuru mbalimbali, ambao hawakuhudhuria vita vya Tabuk), kama vile Nabii Musa -Alaihis Salaam- alipomuacha ndugu yake Harun -Alaihis Salaam- kuwa khalifa wa watu wake Bani Israel wakati alipokwenda Miiqat, wala hayakuwa makusudio ya hadithi hii (kutaja) Uimamu na Ukhalifa (wa Ally kwa waislamu wote), kama wanavyodai hilo Mashia (Ithnaasharia)[(79)].

Na Imam Muslim amepokea hadithi kwa sanadi yake mpaka kwa Ally -Allaah amridhie- amesema: **Naapa kwa yule ambaye ameipasua tumba/mbegu (ya mmea), na amewaumba watu, hakika hiyo ni ahadi ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kwangu mimi, (Mtume) asiyejua kusoma wala kuandika: [kwamba hanipendi mimi isipokuwa (aliye) Muumini na hanichukii**

---

[77]- Tazama kitabu: [Al-Bidaayat wan-Nihaayat] (Jz. 7, Uk. 242).
[78]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari] (3706) na [Sahihi Muslim] (3404).
[79]- Ili kuifahamu vizuri hadithi hii rejea kitabu: [Minhaaju Ssunna] (Jz. 7, Uk. 325).

mimi isipokuwa (aliye) mnafiki][80]**.** Hii ni hadithi nyingine ikielezea nafasi na cheo chake, mpaka imejaaliwa kumpenda yeye ni alama ya Imani na kumchukia ni alama ya unafiki.

Bali siku moja Ally -Allaah amridhie- alikuwa amelala chini kwenye mchanga, Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuja akaanza kumpangusa huku akisema:

"Simama, Ewe Abu Turaab, simama, ewe Abu Turaab"[81]**.**

Na jina hili (Abu Turaab) ni katika majina (Kun-ya) ambayo yeye mwenyewe Ally alikuwa analipenda sana.

[80]- Tazama kitabu: [Sahihi Muslim], (131).
[81]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari], (441) na [Muslim], (2409).

KIPAMBANUZI CHA PILI

KUBAINISHA UHUSIANO MZURI BAINA YA MAKHALIFA WATATU WATATU ABUBAKAR, OMAR NA UTHMAN -Allaah amridhie-

NUKTA YA KWANZA
ALLY KUMSIFIA ABUBAKAR NA OMAR -ALLAAH AWARIDHIE-

Mtu yeyote mwenye kufuatilia historia (sera) ya Khalifa Ally Bin Abi Twalib na uhusiano wake pamoja na Makhalifa hao wawili Abubakar na Omar, atadiriki ni kiasi gani cha mapenzi na udugu uliopo baina yao, na aliendelea kuwatekelezea haki zao baada ya kufariki kwao, haya ndiyo ambayo yamehifadhiwa na vitabu vyetu vya Historia, Hadithi na Tafsiri.

Amepokea Imam Ahmad katika Musnad yake kwamba -Ally Allaah amridhie- alimwambia Abu Juhfa: **"Ewe Abu Juhaifa, je, nisikwambie mbora wa Umma huu baada ya Mtume wake? Amesema: nikasema: kwanini (niambie). Amesema (Abu Juhfa): Na sikuwa mimi naona kuna mtu yeyote ni bora zaidi yake, Akasema (Ally): "Mbora wa Umma huu baada ya Mtume wake ni Abubakar, na baada yake ni Omar, na baada yao ni mtu mwingine wa tatu na wala hakumtaja"**[82].

Haya ni maneno ya wazi kabisa kutoka kwa Ally kwamba Abubakar na Omar ni watu bora katika Umma huu baada ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie-.

Ametaja Imam Ddhahabi -Allaah amrehemu- kwamba Ally -Allaah amridhie- amesema: **"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alimuamrisha Abubakar awaswalishe watu, na mimi nilikuwepo na wala sikuwa mgonjwa. Basi tukamridhia kwa ajili ya Dunia yetu (kuwa khalifa) yule aliyeridhiwa na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kwa ajili ya Dini yetu"**[83].

---

[82]- Tazama kitabu: [Musnad Ahmad] (835). Sanadi yake ni sahihi kwa sharti la Muslim.
[83]- Tazama kitabu: [Tareikhul Islaam] (Jz. 3, Uk. 111).

Na miongoni mwa maneno ambayo Ally Bin Abi Twalib -Allaah amridhie- alikuwa anayakariri sana juu ya mimbari huko mji wa Kufa ni: **"Mbora wa Umma huu baada ya Mtume wake ni Abubakar kisha Omar"**[84].

Pia imethibiti kutoka kwake ya kwamba alikuwa anampinga vikali yule ambaye atamfadhilisha/atamtanguliza yeye zaidi kuliko Abubakar na Omar, na anamuahidi kwa kumuadhibu, alikuwa akisema: **"Sitompata yeyote anayenitanguliza mimi zaidi kuliko Abubakar na Omar isipokuwa nitamchapa mijeledi (kama) anavyochapwa mwenye kuzua uongo"**[85].

Angalia, pamoja na hali ya mji wa Kufa inajulikana kwa fitna na kutukanwa makhalifa watatu (Abubakar, Omar na Uthman), lakini bado yeye alikuwa anakithirisha kuwasifia katika khutba zake, hilo ni kwa sababu ya kuwajibu wazushi. Na mara nyingi Ally alionekana kuvaa kikoti/kizibao, akaulizwa: Ewe Amiirul Muuminin, (mbona) unakithirisha sana kuvaa nguo hii? Akajibu: **"Ndio, hakika amenivalisha mimi nguo hii rafiki yangu mwandani Omar Ibnul Khattwaab, alimtakasia Allaah (moyo wake) na Allaah akamuongoza, kisha akalia"**.

Amesema Imam Sha'bi -Allaah amrehemuu-: amesema Ally Bin Abi Twalib -Allaah amridhie-:

"وَمَا نُبْعِدُ أَنَّ السَّكِينَةَ تَنْطِقُ عَلَى لِسَانِ عُمَرَ"

"Hatuoni ni jambo la mbali, kuwa utulivu (ulio kwenye moyo wa) Omar, unadhihiri/unatamkwa kwenye ulimi wake"[86].

Hivi ndivyo yalivyokuwa mahusiano baina ya Ally, Abubakar na Omar -Allaah awaridhie-, hakika yalikuwa ni mahusiano ya kiudugu na mapenzi, si kama wanavyodai watu wazushi waovu, ambao wanaenda mbio katika kuwafarakanisha waislamu kwa kutunga riwaya mbalimbali za uwongo, ambazo wamezijaza ndani ya vitabu vyao.

---

[84]- Tazama kitabu: [Musnad Ahmad] (Jz. 2, Uk. 562).
[85]- Tazama kitabu: [As Sunnah] (1219). Na ameisahihisha sheikh Albani katika [Dhilaalul Janna].
[86]- Tazama kitabu: [Musnad Ahmad] (Jz. 310), [At-Twabaraani] (8827) na Mu'jamul Kabiir.

Na miongoni mwa jambo zuri hapa kulitaja ni lile ambalo limepokewa ndani ya vitabu vya Shia kwamba Othman -Allaah amridhie- yeye ndiye aliyenunua Dir-i[87] ya Ally ili apate pesa za mahari ya Fatma.

"Basi nikaenda kumuuzia Uthman, kwa Dirham Mia nne nyeusi za Hijri, wakati nilipochukua dirham (pesa) hizo kutoka kwake, na kumkabidhi yeye Dir-i, akasema: [Ewe Abul Hasan (anamkusudia Ally), sikuwa mimi ni mwenye kustahiki zaidi (kuvaa) Dir-i hii kulliko wewe, na wewe unastahiki zaidi (kuchukua) hizo Dirham kuliko mimi, nikasema (Ally): kwanini? Akasema (Uthman): Hii Dir-i ni mimi nimekupa wewe zawadi, (amesema Ally): nikachukua Dir-i na Dirham nikaenda kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na nikaviweka mbele yake, kisha nikamsimulia yeye vile ilivyokuwa kuhusiana na Uthman, akamwombea yeye kheri"[88].

Angalia jinsi gani ya ukweli wa mapenzi haya baina ya watu wawili na kina cha udugu wao, na wala usistaajabu mambo haya kutajwa na vitabu vyao wenyewe, kwa sababu hii ndio asili ya uhusiano kati ya Ally na Makhalifa wengine wote -Allaah awaridhie-.

---

[87]- Dir-I ni kanzu ya chuma inayovaliwa vitani ili kujikinga na silaha.

[88]- Tazama kitabu: [Al-Manaaqib], (Uk. 252-253) cha Khawarizmi. Chapa ya Najaf, na kitabu: [Kashful Ghumma], (Jz. 1, Uk. 359) cha Arbiliy, na [Bihaarul Anwaar], (Jz. 39, Uk. 40) cha Al-Majlis, chapa ya Iran.

NUKTA YA PILI
KUOANA NA KUWAITA (WANAWE) MAJINA YA MAKHALIFA (HAO WATATU)

Miongoni mwa ushahidi wa nguvu ya uhusiano na ukweli wa mapenzi kati ya Ahlul Bayt na Makhalifa (Abubakar, Omar na Uthman), ni kuoana na (kuchanganyikana) Nasaba (zao), kwa sababu mtu hawezi kumuozesha binti yake au dada yake kwa mtu asiyempenda, achilia mbali yule anayemfanyia uadui na kumuona yeye kuwa ni kafiri.

Hakika Maswahaba wengi wameoa kwenye nyumba za Ahlu Bayt na wao pia wameoa kwao (wasiokuwa Ahlul Bayt), na hilo ni kwa makubaliano ya vitabu vya kutegemewa vya Shia na Sunnah.

Na jambo zuri katika mlango huu ni kwamba Makhalifa wanne waongofu, wote ni wakweze Mtume Swala na -Salamu zimshukie-, kwa sababu yeye Mtume amemuoa Aisha (mama wa waumini), binti wa Abubakar Swiddiiq, pia amemuoa Hafsa (mama wa waumini), binti wa Omar, kadhaalika Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alimuozesha Uthman binti zake wawili Ruqayya kisha Ummu Kulthum (baada ya kufariki wa kwanza), Ama Fatma alimuozesha Ally Bin Abi Twalib -Allaah awaridhie-.

Amesema Ibn Taymiyyah -Allaah amrehemu-: **"Ama kumuozesha kwake Fatma hiyo ni fadhila kwa Ally, kama ilivyokuwa kumuozesha kwake Uthman binti zake wawili, hiyo ni fadhila kwa Uthman, kwa ajili hiyo aliitwa Dhan-Nuurain (mwenye nuru mbili), na vilevile kumuoa kwake binti wa Abubakar na Omar -Allaah awaridhie- ni fadhila kwao, kwa hiyo Makhalifa wote wanne ni wakweze Mtume -Swala na Salamu zimshukie-"**[89].

[89]- Tazama kitabu: [Minhaaju Ssunna], (Jz. 4, Uk. 36).

Amesema sheikh Swafiiyyu Rrahman Al-Mubaakfuuriy -Allaah amrehemu-

"Muelekeo wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- katika kufanya Ukwe kwa Abubakar na Omar, kwa sababu ya kuwaoa kwake Aisha na Hafsa, kadhaalika kumuozesha kwake Ally Bin Abi Twalib binti yake Fatma, na kumuozesha kwake Uthman Bin Affaa binti yake Ruqayya kisha Ummu Kulthum, unafahamisha kwamba yeye anataka nyuma ya jambo hilo, kuimarisha uhusiano pamoja na watu hao wanne, (watu ambao) ambao umefahamika mtihani wao, na kujitoa kwao kwa ajili ya (kuunusuru) Uislamu, katika kipindi cha misukosuko mingi uliyopitia, na Allaah akataka uvuke kwa salama, na ilikuwa miongoni mwa mila za Waarabu ni kuheshimu mahusiano yaliyopatikana kwa sababu ya kuozeshana. Hakika kulikuwa kuozeshana ni mmoja kati ya milango ya kuleta mahusiano baina ya koo/familia mbalimbali, na walikuwa wanaona kufanyiana uadui baina pande mbili ambazo wameozeshan ni aibu na fedheha kwenye nafsi zao"[90].

OMAR IBNUL KHATTWAAB KUMUOA UMMU KULTHUM BINT ALLY -Allaah amridhie-

Hakika Omar Al-Farouq -Allaah amridhie- alimuoa Ummu Kulthum -Allaah amridhie- mtoto wa Ally Bin Abi Twalib na Fatma binti wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, na akazaa nae watoto wawili, Zaid Bin Omar na Ruqayya Bint Omar, bali ndoa hii ni maarufu katika vitabu vya Ahlus Sunna na Shia, na wameikubali wanahistoria wote (kwamba tukio hili ni kweli).

"Omar Ibnul Khattwaab alipeleka posa kwa Ally Bin Abi Twalib ya kutaka kumuoa binti yake Ummu Kulthum, Ally akamjibu kuwa (binti yake) bado ni mdogo, watu wakamwambia Omar, (Ally) amekataa m-bembeleze, kisha akamposa tena, Ally akamwambia: bado ni mdogo, (akasema) Omar: hakika mimi nitaichunga heshima yake kuliko mtu mwingine yeyote, yeye kwangu mimi ni mwenye heshima kubwa, Ally akamwambia: nitamleta kwako (umuangalie), ukimridhia basi nitakuozesha, (Ally) akamtuma binti yake kwenda kwa Omar na

[90]- Tazama: [Ar Rahiiqul makhtuum] (Uk. 628).

blanket, akamwambia: (nenda) ukamwambie Omar, hili ndio blanket nililokwambia, (kisha) Omar akamjibu: mwambie (baba yako) nimeliridhia, kisha Omar akaenda kukaa pamoja na Muhajirina katika raudhwa (sehemu ambayo walikuwa wanakusanyika hapo Muhajirina wa mwanzo) akasema: nipongezeni kwa kusema: [mkae kwa amani na mpate watoto], wakamuuliza: kwa sababu gani ewe Amirul muuminiin, akasema: nimemuoa Ummu Kulthum Binti Ally… na alimuoa kwa mahari Dirham elfu arobaini, kisha akazaliwa Zaid Bin Omar (anaitwa Zaid mkubwa) na Ruqayya"[(91)].

Haya, kama Omar aliritadi, mnafiki au amempora Ally ukhalifa (kama wanavyodai Shia), iweje Ally huyo huyo anamuozeshe binti yake kwa mtu huyo dhalimu?! Je huku si kumkejeli Ally -Allaah amridhie?!

Na kama alimuozesha binti yake huyo kwa Omar kwa sababu ya kumuogopa Omar yeye (kama wanavyodai Shia Ithnaasharia), basi uko wapi ule ushujaa ambao amesifika nao Ally Allaah amridhie?.

Halafu vipi Ummu Kulthum aridhie kuolewa na kuishi pamoja na mtu ambaye amempiga mama yake, akamvunja mbavu zake na mpaka kuiharibu mimba yake[(92)]?! Je hii sio dalili kuwa riwaya zenu ni za uwongo?

Na miongoni mwa dalili ya Ally na familia kuwapendaa Masheikh wawili (Abubakar na Omar) ni kuwaita watoto wao majina ya Abubakar na Omar.

---

[91]- Tazama kitabu: [Twabaqaatu Ibn Saad] (Uk. 340), [Taareikhu Ttwabari], (Jz. 5, Uk. 16), [Usdul Ghaaba – Baabul Kaaf] (7587), [Al-Bidaaya wan-Nihaaya], (Jz. 7, Uk. 139), [An-Nasab walmuswaahara baina Ahlil Bayt was-Swahaba], (Uk. 114-117) cha Abu Muadh As-Sayyid.

[92]- Kisa hiki ni cha uwongo (kwamba Omar alivamia nyuma ya Ally, akampiga Ally na kum-bamiza Fatma nyuma ya mlango mpaka akamvunja mbavu zake na kusababisha kuharibika kwa mimba yake), mashia wamekitunga ili kumtia dosari Khalifa wa pili Omar ili wapate njia ya kumlaani. Kwa faida zaidi angalia: [Minhaajus Sunna], (Jz. 4, Uk. 493) cha Ibn Taymiyya. Bali wapo miongoni mwa Maulamaa wao wamepinga kisa hicho, mfano Muhammad Hussein Aal Kaashiful Ghitwaa katika kitabu chake: [Jannatul Ma-waa] (Uk. 63) na Muhammad Hussein Fadhlullaah (Mlebanoni), tazama tovuti: https//www.youtube.com/watch.

Wa kwanza wao ni Ally Bin Abi Twalib -Allaah amridhie- ambaye alimuita mmoja wa watoto wake jina la Abubakar, huu ni ushahidi juu ya upendo, udugu, heshima na kumthamini kwake Abubakar -Allaah amridhie-, na jambo la umuhimu kutajwa ni kwamba mtoto wake huyu alizaliwa baada tu ya Abubakar kupata Ukhalifa na Uimamu.

Na hapa tutataja jumla ya watu wakubwa katika Ahlu-Bayt waliwapa watoto wao majina ya makhalifa hao wawili Abubakar na Omar, na majina hayo yameandikwa na vitabu tegemezi vya Ahlus Sunnah na Shia.

Ambao majina yao ni Abubakar[93]:

- ⇒ Abubakar Bin Ally Bin Abi Twalib.
- ⇒ Abubakar Bin Hassan Bin Ally Bin Abi Twalib.
- ⇒ Abubakar Bin Hussein Bin Ally Bin Abi Twalib.
- ⇒ Abubakar Ally Bin Mussa (Al-Kaadhim) Bin Jafar (As-Saadiq).
- ⇒ Abubakar Bin Abdillaah Bin Jafar Bin Abi Twalib.

Ambao majina yao ni Omar[94]:

- ⇒ Omar Al-Atraf Bin Ally Bin Abi Twalib.
- ⇒ Omar Bin Hassan Bin Ally Bin Abi Twalib.
- ⇒ Omar Al-Ashraf Bin Ally Zainul ‘Abidiin IBin Hussein
- ⇒ Omar Bin Yahya Bin Hussein Bin Zaid As-Shahid Bin Ally Bin Hussein Bin Ally Bin Abi Twalib.
- ⇒ Omar Bin Mussa Al-Kaadhim Bin Jafar As-Swaadiq.

---

[93]- **Tazama vitabu vya Sunna:** [At-Twabaqaat] (Jz. 3, Uk. 14) cha Ibn Saad [Taareikhu Ttwabari], (Jz 3, Uk 162), [Al-Bidaaya wan-Nihaaya] (Jz. 8, Uk. 189) na [Siyar A’laamin Nubalaa] (Jz. 3, Uk. 279). **Ama vitabu vya Shia:** [Al-Irshaad] (Jz. 2 Uk. 125) cha Al-Mufiid, [Muntahal Aamal] (Jz. 1, Uk. 261) cha Al-Qummi, [Taareikhul Ya’quubi], (Jz. 2, Uk. 137), [Kashful Ghumma], (Jz. 2, Uk. 286) cha Abul Hassan Al-Irbili, na [Maqaatilu Ttwaalibin] (Uk. 562).

[94]- **Vitabu vya Suuna:** [Al-Bidaaya wan-Nihaaya] (Jz. 9, Uk. 104), na [Siyar A’laamin Nubalaa] (Jz. 4, Uk. 34) na [Jamharatu Ansaabil ‘Arabi] (Uk. 35) cha Ibn Hazmi. **Ama vitabu vya Shia:** [Al-Irshaad] (Jz. 1 Uk. 354) cha Al-Mufiid, [Muntahal Aamal] (Jz. 1, Uk. 261) cha Al-Qummi, [Bihaarul Anwaar] (Jz. 42, Uk. 120) cha Al-Majlis, [Kashful Ghumma] (Jz. 2, Uk. 24) cha Abul Hassan Al-Irbili, na [Umdatu Ttwaalib] (Uk. 116) katika Hamishi. Cha Ibn ‘Ammba, [Qaamus Rrijaal] (Uk. 83) cha Tustari, na [Al-Anwaaru Nnu’maaniyya] (Jz. 1, Uk. 269) cha Al-Jazaairi.

NUKTA YA TATU
KUSIFIWA ABUBAKAR NA OMAR NDANI YA 'NAHJUL BALAAGHA'

Kitabu (Nahjul Balaagha) chenye kunasibishwa na Ally Bin Abi Twalib -Allaah amridhie-, ambacho kimekusanywa na Sharif Ar-Radhwiy[(95)], huzingatiwa ni chanzo kikubwa cha Dini ya Shia, kwao ni kitabu chenye mvuto na kutiliwa umuhimu mkubwa, na ushahidi wa hilo ni kupatikana Maulamaa wengi wa Kishia walio kisherehesha kitabu hicho na wengine kufanya (sherhe fupi fupi). Achilia mbali kuwepo kwa tarjama ya kitabu hicho kwa lugha mbalimbali, pia kurekebishwa mkusanyaji wake kitabu.

Kwa hiyo sisi katika kukamilisha kitabu chetu hichi tutazitaja riwaya chache zilizo ndani ya kitabu hicho zilizopokewa kutoka kwa Ally -Allaah amridhie- akimsifu Abubakar na Omar -Allaah awaridhie-, miongoni mwa hizo: **"Akawatawalia wao Gavana/Mtawala ambaye alinyoosha (mambo) na alisimama imara, mpaka Dini ikatulizana na kuenea"[96].**

Amesema Ibn Abil Hadiid: **"Gavana huyo ni Omar Ibnul khatwaab -Allaah amridhie-, na maneno hayo ni kutoka katika Khutba yake ndefu aliyohutubia katika masiku za ukhalifa wake"[97].**

Pia amesema: **"Aliicha fitna, akasimamisha Sunnah, ameondoka hali ya kuwa ni msafi wa nguo, mchache wa dosari, alipatia kheri zake na alizitangulia shari zake, ametekeleza kwa Allaah utiifu wake, na akamcha yeye ukwe wa kumcha"[(98)].**

---

[95]- Mashia wanaamini kwamba mtunzi wa kitabu hiki na msemaji wake ni Ally Bin Abi Twalib, lakini si kweli, na ukweli ni kwa kwamba mtunzi wake ni Sharif Rradhwiy, aliyefariki mwaka (406H), na Ally -Allaah amridhie- amefariki mwaka (40H), na wala hakuna sanadi yenye kuungana mpaka kwa Ally. Ama makusudio ya kunukuu ndani ya kitabu hiki, ni katika njia ya kumlazimisha mpinzani wetu (Shia) kwa kumtajia kitabu ambacho yeye anakiamini. Na ukitaka ziada kuhusu kitabu hichi soma: [Kutub Haddhara minhal Ulamaa] (Jz. 2, Uk. 251) cha Sheikh Mash-hur Hassan.

[96]- Tazama: [Nahju al-Balagha] (Uk. 557). Daarul kitaabil 'Arabi. Tahkiki ya Dr. Swabhi As-Swaalih.

[97]- Tazama kitabu: [Sharhu Nahju al-Balagha], (Jz. 4, Uk. 107). Cha Ibn Abil Hadid.

[98]- Tazama: [Nahju al-Balagha], (Uk. 557). Daarul kitaabil 'Arabi. Tahakiki ya Dr. Swabhi.

Bali Mshia Ibn Abil Hadiid amefafanua zaidi kwa kusema: **"Na huyo fulani[99] ni Omar Ibnul Khattwaab -Allaah amridhie- , na nimefanikiwa kuipata nakala ya mwandiko wa Ar-Radhwiy Abul Hassan aliyekusanya kitabu (Nahj al-Balagha), na chini na neno fulani (maana yake ni) Omar, nikamuuliza An-Naqib Abu Ja'far Yahya Bin Abi Zaid Al-'Alawiy (kuhusu tafsiri hiyo) akaniambia: huyo ni Omar, nikamuuliza: (Je), Amirul Muuminin alimsifia yeye kwa sifa zote hizi? Akasema: ndio"[100].**

Pia imetajwa habari ya Omar kumtaka ushauri Ally ili atoke yeye mwenyewe (pamoja na jeshi) kwenda kupigana vita huko Roma, na Ally akamwambia: **"Ukienda utakapoenda wewe mwenyewe kwa adui, kisha ukakutana nae na ukafikwa na matatizo, Waislamu hawatakuwa na mlinzi wowote ukiwa wewe uko mbali nao, na watakosa sehemu ambayo watarejea (kwa mambo mbalimbali), basi mtume kwao mtu shujaa, na afuatane pamoja na wapiganaji washauri, ikiwa Allaah atawapa ushindi (hivyo) ndivyo tunavyotarajia, na likiwa jambo lingine (wakishindwa), basi utakuwa wewe ndio nguo ya Waislamu (sitara yao), na ndio marejeo yao"[101].**

---

[99]- Hapa anafafanua kwamba Shia wanawaita Abubakar na Omar (Fulani na Fulani), wanaficha majina yao, lakini wapo wanachuoni wao waliobainisha maana yake, kama anavyosema hapa mwanachuoni wao Abil Hadid.

[100]- Tazama kitabu: [Sharhu Nahju al-Balagha], (Jz. 2, Uk. 505).

[101]- Tazama: [Nahju al-Balagha], (Uk. 193). Chapa ya Daarul kitaabil 'Arabi. Tahakiki Dr. Swabhi.

NUKTA YA NNE
ALLY KUMPA BAI'A ABUBAKAR SIDDIIQ -Allaah amridhie-

Mtume -Swala na Salamu zimshukie- baada ya kufikisha risala aliyotumwa na Mola wake, akatekeleza amana, na kuunasihi umma huu kwa ukamilifu na kubainisha kulikotimia, alifariki na kwenda kukutana na Mola wake.
Wakati watu wakiwa katika huzuni na vilio, tahamaki alikuja Abubakar Siddiiq -Allaah amridhie-, hali ya kuwa ni mwenye imani ya yakini iliyo madhubuti, akaufunua mwili wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- akaubusu uso huo mtukufu, kisha akatoka nje, akasema maneno yake yaliyo maarufu, ili waislamu wapate kutulizana, na kuwakumbusha wajibu wao kuhusu risala ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, kisha akapanda kwenye mimbari, akamhimidi Allaah na akamsifu kisha akasema: **[Yule ambaye alikuwa akimuabudu Muhammad, basi Muhammad tayari amekufa, na yule aliyekuwa akimuabudu Allaah, basi Allaah yupo hai wala hatokufa]**, na akaisoma kauli ya Allaah:

﴿ إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُم مَّيِّتُونَ ﴾

"Hakika wewe ni mwenye kufa na wao ni wenye kufa". Surat Az-Zumar/30.

Na kauli yake:

﴿وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ ٱلرُّسُلُ ۚ أَفَإِيْن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ ٱنقَلَبْتُمْ عَلَىٰٓ أَعْقَـٰبِكُمْ ۚ وَمَن يَنقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ فَلَن يَضُرَّ ٱللَّهَ شَيْـًٔا ۗ وَسَيَجْزِى ٱللَّهُ ٱلشَّـٰكِرِينَ﴾

"Hakuwa Muhammad (ni kiumbe aina nyingine), isipokuwa ni Mtume sawa na Mitume wengine waliopita kabla yake, iwapo atakufa au atauawa kwani mtarudi nyuma kwa (kuacha dini yenu). Basi yoyote miongoni mwenu atakayerudi nyuma, yeye hatamdhuru Allaah chochote, (na yule atakaesimama imara juu ya Imani yake) na akamshukuru Mola wake (juu ya neema ya Uislamu) hakika Allaah atamlipa malipo mazuri kabisa"[102]. Watu wakaanza tena kuangua vilio[103].

---

[102]- Surat Aal- Imraan/144.
[103]- Bukhari (1241) na (3668).

Hili ndio tukio kubwa kabisa lililowapata Waislamu tangu kufariki kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- mpaka kusimama kiama, tukio ambalo waumini walijua uimara wa Abubakar Siddiiq, zikaongezeka kwake sifa njema wachilia mbali sifa nyingine ambazo Mtume -Swala na Salamu zimshukie- aliwahi kumsifia katika minasaba mbalimbali.

Kisha baada ya hapo likatokea tukio la Ansar kukusanyika huko Thaqifa, Abubakar Siddiiq -Allaah amridhie- akaenda haraka kuizima fitna ambayo ingepelekea kwenye mpasuko baina ya waislamu na kugawanyika, akawakuta watu wamekusanyika hali ya kuwa rai zao zimetafautiana, (lakini kama kawaida yake) Abubakar Siddiiq, akaongea maneno ambayo watu wote waliafikiana katika rai moja (na kuziacha rai zao), kisha ikatimia kwake Bai'a (kiapo cha utiifu), bila ya mjadala, ugomvi wala shaka yoyote.

Na halikuwa tukio la Thaqifa isipokuwa ni watu wa Madina (Ansar), waliokusanyika kwa ajili ya kujadiliana kadhia za mji wao baada ya tukio hilo kubwa, ikawa jitihada zao ni kuwa atoke kiongozi miongoni mwao, lakini Abubakar Siddiiq -Allaah amridhie- akawabainishia kwamba jambo la uomgozi lipo kwa Makaureishi, watu wote wakafuata kauli yake hali ya kuwa wamenyenyekea. Na haikuwa kuchaguliwa kwake ni mpango alioupanga yeye au Muhajiriina, kama wanavyodai hilo watu wenye chuki dhidi ya Maswahaba, bila ya hoja wala nukuu yoyote yenye kutegemewa.

Kwa hiyo watu wote waliokuwa Thaqifa walimpa yeye Bai'a pamoja na huzuni na mgongano walioupata kwa tukio la kufa Mtume, kutokana na sifa alizokuwa nazo, kwa sababu yeye alikuwa pamoja naye pangoni, **na** ndiye aliyewaswalisha watu wakati wa maradhi ya Mtume kwa ruhusa yake. Na katika asubuhi ya siku ya jumanne ambayo ni siku ya pili tangu kufariki Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kabla ya kuandaa mazishi yake, watu wote katika Muhajirina na Ansar walimiminika kumpa yeye bai'a, na hii ikawa ndio bai'a ya watu wote baada ya kukosekana baadhi yao katika ile bai'a ya Thaqifa[(104)].

[104]- Al-Bidaaya wan-Nihaaya (Jz. 5, Uk. 268).

Imepokewa kutoka kwa Anas -Allaah amridhie-, kwamba yeye aliisikia khutba ya Omar -Allaah amridhie- wakati alipokaa kwenye mimbari, siku ya pili tangu kufariki Mtume -Swala na Salamu zimshukie- , akamshuhudisha Allaah kwa kusema: (Laa ilaaha illallaahu) na hali kuwa Abubakar amenyamaza kimya wala haongei chochote, akasema (Omar): **[Nilitarajia kwamba Mtume wa Allaah -Swala na Salamu zimshukie- atabaki mpaka awe yeye ndiye wa mwisho wetu (kufa), ikiwa Muhammad tayari amekufa, basi Allaah amewajaalieni mbele yenu nuru ambayo mtaitumia katika kuongoka, …… na hakika Abubakar ni rafiki wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, naye ni wa pili katika wawili (waliokuwa pangoni), hakika yeye ni mbora zaidi wa Waislamu katika kusimamia mambo yenu, basi simameni na mpeni yeye bai'a (kiapo cha utiifu)].**

Na lilikuwa kundi miongoni mwao tayari limeshampa yeye bai'a huko Thaqifa Bani Saa'ida, na ikawa bai'a ya watu wote ni (msikitini) katika mimbari.

Amesema Imam Zuhri -Allaah amrehemu- : Imepokewa kutoka kwa Anas Ibn Malik -Allaah amridhie- amesema: Nilimsikia Omar anamwambia Abubakar siku hiyo: **[Panda mimbari],** hakuacha kumwambia mpaka Abubakar akapanda mimbari, kisha watu wote wakampa Bai'a[(105)].

Ikawa wa mwanzo kumpa Bai'a ni wale wakubwa katika Maswahaba wakiongozwa na Ally -Allaah amridhie-, wala yeye hakukataa kumpa Bai'a Abubakar, ama yale waliozua wapokezi wa Shia katika riwaya za uwongo, hizo hazina nafasi yoyote mbele ya Maulamaa wa wahakiki wa hadithi na athari mbalimbali, kwa sababu chimbuko la riwala hizo ni kutoka kwa watu waongo, wenye kutunga hadithi na kubadilisha athari nyingi zilizopokewa[(106)].

---

[105]- Bukhari (7219).

[106]- Kama mfano wa mtu anaeitwa Lut Ibn Yahya Abu Mikhnaf, Hisham Ibn Muhammad Bin Saaib Al-Kalbiy, Zuraara Ibn A'yun, Jabir Al-Ju'fiy na wenzao.

Kwa hiyo Ally alimpa bai'a Abubakar mara mbili, mara ya kwanza ni msikitini katika bai'a ya Maswahaba wote, kama alivyopokea Imam Baihaqi kwa sanadi yake mpaka kwa Abu Saidi Al-Khudri amesema: **"Alipofariki Mtume -Swala na Salamu zimshukie- watu walikusanyika nyumbani kwa Sa'd Bin Ubada, akiwemo Abubakar na Omar -Allaah awaridhie-, amesema: alisimama khatibu wa Ansar akasema: Je, si mnajua kwamba Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuwa miongoni mwa Muhajirina, na khalifa wake ni miongoni mwa Muhajirina, na sisi (watu wa Madina) ni Ansar (watetezi) wa khalifa wake, kama tulivyokuwa Ansar (watetezi) wakati wake. Omar -Allaah amridhie- akasema: [msemaji wenu amesema kweli, lau mngelisema tafauti na hivi tusingewapa bai'a, akaushika mkono wa Abubakar na akasema: Huyu ni swahiba wenu mpeni bai'a, (watu wote) Muhajirina na Ansar (walisimama) kumpa bai'a, kisha Omar na yeye akatoa bai'a, amesema: kisha Abubakar akapanda kwenye mimbari akawatizama watu (waliohudhuria), hakumuona Zubeir, akatuma aitwe, alipofika akamuuliza: Mtoto wa shangazi yake Mtume -Swala na Salamu zimshukie- unataka kuvunja umoja wa Waislamu! Akasema (Zubeir): Hapana lawama (yoyote kwako) ewe khalifa wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, akasimama na akampa bai'a, kisha akatazama nyuso za watu hakumuona Ally, akatuma aitwe, alipokuja alimuuliza: Ewe mkwe wake Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na mtoto wa Ami yake, je unataka kuvunja umoja wa Waislamu! akasema: Hapana lawama (yoyote kwako), ewe khalifa wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- , kisha wakampa bai'a"[107].**

Amesema Ibn Kathir - Allaah amrehemu - **[Sanadi hii ni sahihi, na ndani yake kuna faida kubwa, nayo ni: kwamba bai'a ya Ally ima ilikuwa katika siku ya kwanza, au katika siku ya pili, tangu kufariki Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na hili ni kweli, kwa sababu Ally hakuwahi kuachana na Abubakar Siddiq katika wakati wowote, wala hakuacha kuswali nyuma yake swala yoyote, kisha akaondoka pamoja naye kwenda huko Dhil-Qasswa wakati**

[107]- Al-Baihaqi (Jz. 1, Uk. 143). Na ameisahihisha Ibn Kathir.

abubakar alipotoka nje hali ya kuwa amechomoa upanga wake kwa ajili ya kwenda kupigana na watu walioritadi][108].

Na miongoni mwa ushahidi unaothibitisha mafungamano mazuri baina ya Ally na Abubakar -Allaah awaridhie- ni riwaya aliyoipokea Imam Bukhari kutoka kwa 'Uqba Bin Harith, amesema: **[(Siku moja) Abubakar aliswali swala ya Alasiri, kisha akatoka anatembea, mara akamuona Hassan anacheza na watoto (wenzie), akambeba katika mabega yake na akasema: namtoa fidia baba yangu (kwa ajili yako), wewe umefanana na Mtume wala hujafanana na Ally]**, na hali ya kuwa Ally anacheka[109].

Na bai'a ya mara ya pili, ni baada ya kufariki Fatma -Allaah amridhie- na hii inazingatiwa ni bai'a ya pili ambayo iliondoa simanzi iliyosababishwa na maneno kuhusiana na mirathi (ya Fatma) na suala la ardhi ya Fadak, na namna alivyofanya Abubakar Siddiq katika kutekeleza hukumu ya Mtume -swala na salamu zimshukie-, pale aliposema: **[(Sisi Mitume) haturithiwi, kile tulichokiacha (katika mali) hicho ni sadaka]**[110].

Na tukio hili la bai'a ya pili limetajwa na Maimamu wa hadithi, kama vile Bukhari (3998) na Muslim (1759), na watunzi wa vitabu vya Sunan. Na pia wanachuoni wa Fiqhi wamebainisha kuafikiana mioyo ya Maswahaba katika zama za Abubakar, miongoni mwao alikuwepo Ally Bin Abi Twalib.

Na hapa inabainika uwongo wa riwaya wanazozitaja Shia Ithnaasharia, kwamba Ally Bin Abi Twalib -Allaah amridhie- alikataa kumpa bai'a (kiapo cha utiifu) Abubakar Siddiiq, na hii ni ishara ya wazi kwamba Ally aliunga mkono uongozi wa Abubakar na kuuridhia -Allaah awaridhie-.

108- Tazama kitabu: [Al-Bidaaya wan-Nihaaya], (Jz. 5, Uk. 281).
109- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari], (3542).
110- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari (3712) na Muslim (1759).

Amesema D. Muhammad Al-Fahdaawi (wakati akielezea uadilifu wa Maswahab): “Bali Ally yeye mwenyewe amelisisitiza hili, pale aliposema: **[Tahamaki, nikaona watu wengi wakimiminika kwa Abubakar kwa ajili ya kumpa bai’a]**[111].

Na wakati Ally -Allaah amridhie- alipotaka kumthibitishia Muawiya -Allaah amridhie- juu ya ukhalifa wake alimuandikia barua inasema: **[Hakika wamenipa bai’a (wamenichagua) mimi wale wale ambao walimchagua Abubakar, Omar na Othman, juu ya kile ambacho walimpa bai’a wao, basi hapakuwa na hiyari kwa aliyehudhuria, wala kukataa kwa asiyekuwepo, kwa sababu shura inayozingatiwa ni ya Muhajirina na Ansar, wakikubaliana juu ya mtu na wakamuita kuwa ni imam (kiongozi), linakuwa hilo kwa Allaah ni lenye kuridhiwa, na akitoka yeyote nje ya makubaliano hayo, kwa kukosoa au kuzusha bidaa, basi watamrudisha kwenye lile ambalo ameliacha, na endapo akikataa watampiga yeye juu ya kufuata kwake njia isiyokuwa ya waislamu, na Allaah atamuongoza huko alikoelekea]”**[112].

Pamoja na haya yote, bado kuna Mashia ambao wanapinga bai’a hii ya Ally kwa Abubakar Siddiq, kwa madai ya kwamba ilikuwa ni bai’a ya kulazimishwa na kutenzwa nguvu, lakini mmoja wa wanachuoni wao wa zamani anayeitwa An-Naubakhti ametilia mkazo kwamba jambo lilikuwa kwa ridhaa yake Ally wala hakulazimishwa, amesema: **[Basi kundi kubwa la watu lilikuwa pamoja na Abubakar na Omar, hali ya kukubaliana nao na kuwaridhia]**[113].

Kwa ufupi ni kwamba bai’a hiyo imethibiti na hakuna yeyote mwenye akili timamu anayeweza kupinga, pia ba’ia ya Maswahaba wengine, Ahlul Bayt, na wale waliobaki katika Maswahaba kumi waliobashiriwa pepo, akiwemo Zubeir Ibn ‘Awwam kama ilivyotangulia.

---

[111]- Tazama kitabu: [Nahjul Balaagha] (Uk. 35).
[112]- Tazama kitabu:[Nahjul Balaagha] (366-367). Daarul Kitaabil ‘Arabi. Tahkiki D.Swabhi Sswaalih.
[113]- Tazama kitabu: [Firaqu Sshia], (Uk. 4). Cha An-Naubakhti.

Ally -Allaah amridhie- anakataa Wasia na Uimamu:

Kama tulivyoona kwamba ukhalifa wa Ally -Allaah amridhie- haukuwa kwa Dalili ya wazi ndani ya Qur'an wala Sunnah, bali alichaguliwa kwa shura ya Muhajirina na Ansar, kwa sababu hakuna dalili ya Ukhalifa kwa swahaba yeyote, si Abubakar, Omar, Uthman wala Ally, lakini zilipatikana ishara nyingi zenye nguvu zilizopelekea kutangulizwa Abubakar Siddiiq kuliko Maswahaba wote, kama alivyotangulizwa kuwaswalisha watu katika uhai wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, na wakati huo alikuwepo Omar, Uthman, Ally na Maswahaba wengine wakubwa -Allaah awaridhie-.

Imepokewa kutoka kwa Abdullaahi Bin Omar -Allaah awaridhie- amesema: aliulizwa Omar, kwanini usimchague Khalifa? Akasema: **[Ikiwa nitamchagua Khalifa (kiongozi baada yangu), basi alishatangulia kuchagua yule aliye mbora kuliko mimi (ambaye ni) Abubakar, na nikiacha kumchagua (Khalifa), basi pia aliacha yule aliye mbora kuliko mimi, (ambaye) ni Mtume -Swala na Salamu Zimshukie-]**[114].

Na pia imepokewa kutokwa Abu Juhaifa akasema: Nilimuuliza Ally Bin Abi Twalib, Je, mna nyinyi kitabu (kingine isiyokuwa Qur'an)?

Akasema: **[Hapana, isipokuwa kitabu cha Allaah, au ufahamu aliyopewa muislamu au yaliyomo ndani ya karatasi hii].** Amesema: Basi nikamuuliza: Je, kuna nini ndani ya karatasi hiyo? Akasema: **[Akili, kuwaachilia mateka, na Muislamu hauwawi kwa ajili ya (kumuua) kafiri]**[115].

Hapa Ally Allaah amridhie- anakanusha waziwazi kwamba hakuna wasia wala kitabu chochote alichopewa na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kwa kuhusishwa yeye tu, bila wengine kujua. Pia imekuja katika sahihi Muslim, kutoka kwa Twalha Bin Muswarrif amesema: Nilimuuliza Abdullaah Bin Abi Aufa: **[Hivi Mtume -Swala na Salamu zimshukie- aliusia?].** Akasema: **[Hapana].** Nikasema: **[Basi kwa nini uliwajibishwa wasia kwa**

---

[114]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari] (7218) na [Sahihi Muslim] (1823).

[115]- Tazama kitabu: [Sahihi Bukhari] (111).

Waislamu? Au kwa nini waliamrishwa wasia?]. Akasema: **[Ameusia kushikamna na kitabu cha Allaah 'Azza Wajalla]**[116].

Na ametaja Imam Hakim -Allaah amrehemu- kutoka kwa Sha'bi, kutoka kwa Abu Waail amesema: Ally Bin Abi Twalib -Allaah amridhie- aliulizwa: **[Kwa nini usituchagulie sisi kiongozi (baada yako)?].** Akasema: **[Vipi mimi nimteue kiongozi (baada yangu) na hali ya kuwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- hakumteua kiongozi (baada yake)? Lakini Allaah akitaka kwa watu kheri, atawakusanya katika kheri yao hiyo (atawapa kiongozi bora) baada yangu, kama alivyowakusanya katika kheri yao baada ya kufa Mtume wao (Swala na Salamu zimshukie-)]**[117].

Kadhalika imepokewa kutoka kwa Fudhwail Bin Marzuuq amesema: Nilimsikia Al-Hassan Ibnul Hassan, wakati alipoulizwa na mtu mmoja: **[Hivi Mtume -Swala na Salamu zimshukie- hakusema 'Yule ambaye ananipenda mimi basi na Ally ni kipenzi chake?'].** Akasema: **[Ndio, (amesema hivyo), naapa kwa Allaah, lau Mtume -Swala na Salamu zimshukie- angekusudia uongozi na utawala, angeliwabainishia wao jambo hilo, kwa sababu Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuwa ni mwenye kuwanasihi Waislamu, angesema: 'Enyi watu, huyu ndiye mlinzi na mtawala wenu baada yangu, msikilizeni na mumtii'!. Naapa kwa Allaah, lau Allaah na Mtume wake wangemchagua Ally kwa ajili ya jambo hili na kumfanya kuwa ndiye msimamizi wa Waislamu wote baada yake kisha Ally akaacha kutekeleza amri ya Allaah na Mtume wake, basi angelikuwa Ally ndiye wa mwanzo kuacha amri ya Allaah na Mtume wake]**[118].

---

[116]- Tazama kitabu: [Sahihi Muslim] (1634).

[117]- Tazama kitabu: [Al-Mustadrak] (4524). Na amesema: Hadithi hii sanadi yake ni sahihi.

[118]- Tazama kitabu: [Al-I'tiqaad wal-Hidaaya ilaa Sabiili Rrashaad] (Uk. 499). Ameitaja Imam Al-Bayhaqi kwa sanadi iliyo sahihi.

Hakika makusudio ya utafiti huu wa kuthibitisha kupinga kwake Ally kwamba kuna wasia au kitabu maalumu kilichoandikwa kuhusu Ukhalifa wake, ni kutilia msisitizo juu ya kuwapenda kwake Ally makhalifa wawili Abubakar na Omar -Allaah awaridhie-, ukiongezea mapenzi yake juu yao kama tulitangulia kutaja ndani ya kitabu chetu hiki, na kwamba hakuna chochote baina yao kinachozuia asiwapende na kuwasifia, ama wasia hilo ni jambo la uwongo na uzushi ambao yeye mwenyewe Ally ameupinga.

HITIMISHO

Ewe ndugu yangu msomaji: ni matarajio yangu kwamba umefahamu kupitia maandishi yaliyo ndani ya kitabu chetu hiki, ukaribu uliokuwepo baina ya Maswahaba na Ahlul Bayt (jamaa wa nyumba ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie-), katika kupendana na kusifiana, hasa hasa baina ya Ally Bin Abi Twalib na baina ya, Abubakar na omar -Allaah awaridhie Maswahaba wote-.

Baadhi ya natija tulizopata kupitia utafiti huu:

1. **Maswahaba ni watu wenye cheo kikubwa mbele ya Waislamu wote.**
2. **Makhalifa wema waongofu ndio watu bora baada ya Manabii, na mbora wao zaidi ni Abubakar, kisha Omar, kisha Uthman, kisha Ally.**
3. **Usafi wa mioyo ya Ahlus Sunnah juu ya Maswahaba na Ahlul Bayt.**
4. **Mafungamano yaliyopo baina ya Ally, Abubakar na Omar -Allaah awaridhie- ni mafungamano ya udugu, mapenzi na kuheshimiana.**
5. **Ally -Allaah amridhie- kuwasifu kwake makhalifa wawili (Abubakar na Omar), ni jambo limethibiti kwa ushaidi na dalili nyingi sahihi.**
6. **Mapenzi yaliyopo baina ya Ally, na makhalifa hao wawili yanabatilisha madai ya Shia, (ushia) ambao kudumu kwake kunategemea propaganda ya kwamba baina ya Ally, Abubakar na Omar kuna chuki na ugomvi.**

Huu ndio ukweli na hii ndio historia ambayo wanajitahidi maadui wa Uislamu (Shia) kuibadilisha bali kuipoteza, ili wapate kuwatukana watu ambao Mtume -Swala na Saalamu zimshukie- amewalea, amewafundisha, amewaozesha binti zake na yeye ameoa kwao, lakini Allaah ni mwenye kulishinda jambo lake.

Wabillaahi Ttaufiiq

Na -Swala na Salamu zimshukie- Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Mwandishi:
Ally Bin Abdillaahi Al-Ammaari
20/ramadhani/1429H.